Elimu ya Dini ya Kiislamu

Madrasa na Shule za Msingi

# Kitabu cha Nne



Islamic Propagation Centre

# Elimu ya Dini ya Kiislamu

Madrasa na Shule za Msingi

**Kitabu-IV**

Islamic Propagation Center

Toleo la Pili 2007

Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.

©Hakimiliki 2007 IPC

Elimu ya Dini ya Kiislamu
Madrasa na Shule za Msingi
Kitabu cha Nne

Wachapaji/Wasambazaji
Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.
Chapisho la Pili, 09, Januari, 2007
Nakala 1000

Kimetayarishwa na Islamic Propagation Centre
P.O.BOX 55105, simu 022-22450069.

Usanifu wa kurasa na Michoro
Idd S. Kikong'ona
Katti-Ka-Batembo
Educomix Associates Ltd, Dar es Salaam.

## YALIYOMO

**SOMO LA KWANZA**

Kusoma na Kutafsiri....1
- Ujumbe wa Suratil-Fat-ha....2
- Ujumbe wa Suratul-Nnaas....4
- Ujumbe wa Suratul Falaq....6
- Ujumbe wa Suratul-Ikhlas....7
- Ujumbe wa Suratul-Lahab....8
- Ujumbe wa Surat-Nasr....9
- Ujumbe wa Suratul Kaafiruun....10
- Ujumbe wa Suratul-Kawthar....11
- Ujumbe wa Suratul-Maun....12
- Ujumbe wa Suratul-Quraysh....14
- Ujumbe wa Suratul-Fyl....16
- Ujumbe wa Suratul-Humazah....18
- Ujumbe wa Suratul-'Asr....20
- Ujumbe wa Suratul-Takaathur....22
- Ujumbe wa Suratul-Qaari'ah....24
- Ujumbe wa Suratul-'Adiyat....27
- Ujumbe wa Suratul-Zilzal....28

Zoezi la kwanza....30

**SOMO LA PILI**

Sifa za Allah (s.w)....31

Matumizi ya majina ya Allah (s.w)....46

Sifa za Allah (s.w) katika Qur-an....48
- Ayatul-Qursiyyu....48
- Suratul-Hadyd....49
- Suratul-Hashr....51
- Suratul-Ikhlas....52

Maana ya Kumuamini Allah (s.w) katika maisha ya kila siku....53

Kumshirikisha Allah (s.w)....53
- (i) Shirki ya Dhati....54
- (ii) Shirki ya Sifa....54
- (iii) Shirki ya Mamlaka....54
- (iv) Shirki ya Hukumu....55

Zoezi la pili....56

## SOMO LA TATU

Twahara..............57
Kutayammamu..............57
Kusimamisha Swala..............60
Swala ya Jamaa..............66
Zakat..............71
Aina za mali zinazotolewa Zakat..............72
Wanaostahiki kupewa Zakat..............72
Funga ya Ramadhani..............73
Nguzo za funga..............74
Yanayobatilisha funga..............74
Yasiyobatilisha funga..............75
Zoezi la Tatu..............76

## SOMO LA NNE

Vazi lenye Sitara..............77
Faida ya Kuvaa Hijab..............81
Michezo katika Uislamu..............82
Michezo ya Laghwi..............85
Zoezi la Nne ..............86

## SOMO LA TANO

Uslamu wakati wa Mtume (s.a.w)..............87
Kuanzisha Dola ya Kiislamu Madinah..............87
Msikiti wa Qubah..............88
Msikiti Mkuu wa Madinah..............88
Kuunganisha Udugu..............90
Mkataba wa Madinah..............92
Kutokeza kwa kundi la Wanafiki ..............93
Mabadiliko ya Qibla na athari zake..............93
Upinzani dhidi ya dola ya kiislamu..............95
Vita vya Badr..............95
Vita vya Uhd..............97
Vita vya Ahzab..............100
Mkataba wa Hudaibiya..............101
Vita vya Khaibar..............103
Vita vya Muttah..............103
Kukombolewa kwa Makkah..............104
Msafara wa Tabuk..............104
Hija ya kuaga na kutawafu Mtume (s.a.w)..............105
Zoezi la Tano ..............108

## Neno la Awali

Shukrani zote njema anastahiki Allah (s.w). Rehema na Amani zimwendee Mtume Muhammad (s.a.w) na wale wote wanaofuata njia yake.

Tunamshukuru Allah (s.w) kwa kutuwafikisha kutoa kitabu hiki cha Nne kwa ajili ya watoto wetu wa Madrasa na Shule za msingi. Kitabu hiki ni katika mfululizo wa vitabu saba kwa ajili ya Madrasa zetu na shule za msingi.

Vitabu hivi vimeandaliwa kwa lengo la kuwawezesha watoto wa kiislamu kupata elimu ya msingi ya dini yao katika fani za Qur'an, Tawhid, fiqh, akhlaq na tarekh.

Tunamuomba Allah atujaalie kulifikia lengo lililokusudiwa na atujaalie sisi na watoto wetu kuwa makhalifa wa Allah (s.w).

Wabillah Tawfiq

Mwalimu Mratibu
Islamic Propagation Centre

# Somo la 1. Qur'an

## KUSOMA NA TAFSIRI

### Kuhifadhi Qur'an

Mwanafunzi darasa la nne anatarajiwa aweze kusoma kwa ufasaha na kuhifadhi sura katika Juzuu ya 28/29 kuanzia Suratul-Talaq (65) mpaka Surat-Nuhu (71)

### Kusoma na Kutafsiri

Mwanafunzi wa darasa la IV anatarajiwa pia aweze kuhifadhi tafsiri ya Suratul-Jinni (72) hadi Suratul-Mursala (77). Mwanafunzi atumie msahafu wa tafsiri ya Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy.

### Ujumbe wa Qur'an

Lengo la kushushwa Qur'an na vitabu vingine vya Allah (s.w) ni kumuongoza mwanaadamu katika maisha yake yote. Hivyo ni wajibu wa Muislamu kusoma Qur'an kwa mazingatio ili aweze kupata ujumbe uliomo ndani. Baada ya muumini kupata ujumbe wa Qur-an huutekeleza katika maisha yake ya kila siku. Mwanafunzi wa darasa la nne anatarajiwa aweze kuubainisha ujumbe wa Suratul-Fat-ha hadi Suratul-Zilzala.

ina aya 7 | **Suuratul Fat-ha 1** | Makka

| | |
|---|---|
| 1.Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma mwenye kurehemu. | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 2.Sifa njema zote zinamstahikia Allah. Mola wa viumbe vyote. | الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١﴾ |
| 3.Mwingi wa Rehma, mwenye kurehemu. | الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ ﴿٢﴾ |

| | |
|---|---|
| 4.Mwenye kumiliki siku ya malipo. | مٰلِكِ يَوْمِ الدِّيْنِ ﴿٣﴾ |
| 5.Wewe tu ndiye tunayekuabudu na wewe tu ndiye tunayekuomba msaada. | اِيَّاكَ نَعْبُدُ وَاِيَّاكَ نَسْتَعِيْنُ ﴿٤﴾ |
| 6.Tuongoze katika njia iliyonyooka | اِهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيْمَ ﴿٥﴾ |
| 7.Njia ya wale uliowaneemesha, sio ya wale waliokasirikiwa, wala ya wale waliopotea. | صِرَاطَ الَّذِيْنَ اَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوْبِ عَلَيْهِمْ وَلَا الضَّآلِّيْنَ ﴿٧﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Fat-ha**

1.**Kuanza kila jambo kwa** "*Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim*"

Sura hii ndio ya kwanza katika Msahafu na aya yake ya kwanza imekuwa ni "Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim". Hivyo sura hii inatufundisha kuwa awali ya kila jambo jema tunalolifanya iwe ni "*Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim*".

Allah (s.w) analibariki jambo jema lililoanza kwa "*Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim*". Kinyume chake lolote lililoanzwa bila ya "*Bismillahir-Rahmaanir-Rahiim*" halirehemewi na Allah (s.w).

**2.Kumsifu na Kumtukuza Allah** (s.w)

Sura inatufundisha vile vile kuwa Waisalmu tunapaswa kumtukuza na kumsifu Allah (s.w) pekee kwa sababu:

(a) Yeye ndiye Mola wetu aliyetuumba, akatulea na kutukuza mpaka tukafikia umri huu tulionao.

(b) Yeye ndiye aliyetuneemesha kwa kutupa uhai na kila kitu tulichonacho. Vitu vyote tulivyo navyo ikiwa ni pamoja na afya zetu, akili zetu, wazazi wetu, ndugu zetu, mali zetu n.k. ametupa Allah (s.w).

(c) Yeye ndiye Mfalme aliyejuu ya wafalme wote tunaowajua hapa ulimwenguni. Na atakuwa mfalme Peke yake siku ya Kiyama.

### 3.Kumuabudu na Kumtegemea Allah Pekee

Kwa sababu hizo zilizotajwa hapo juu Waislamu tunalazimika kumuabudu Allah (s.w) peke yake. Kumuabudu Allah (s.w) ni kumtii kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha yale yote aliyotukataza.

Pia tunajifunza kuwa Waislamu tunalazimika kutaka msaada wa Allah (s.w) katika kila jambo tunalolihitaji. Kwa ujumla tunatakiwa tutie juhudi katika kuyaendea mahitaji yetu kisha tuombe msaada wa Allah (s.w). Bila shaka tutakuwa ni wenye kufanikiwa, kwani Allah (s.w) ni muweza juu ya kila kitu.

### 4.Kuomba Mwongozo

Waislamu tunalazimika kumuomba Allah (s.w) atuongeze katika njia iliyonyooka. Njia iliyonyooka ni Uislamu. Tunajifunza kuwa ili Allah (s.w) atuongeze katika njia ya Uislamu hatuna budi:-

(a) Kuiga mwenendo wa wale aliowaneemesha Allah (s.w) ambao ni:

- ☞ Mitume.
- ☞ Maswidiq – waliowasadikisha Mitume (Maswahaba na Mitume).
- ☞ Mashahidi – Waliosimama kidete kupigania dini ya Allah kwa mali zao na nafsi zao mpaka wakafa katika uwanja wa mapambano.
- ☞ Maswalihi – Watu wema walioishi maisha yao yote kwa kufuata maamrisho ya Allah (s.w) na kuacha makatazo yake.

(b) Kujiepusha na mwenendo wa wale waliokasirikiwa na Allah (s.w). Waliokasirikiwa na Allah (s.w) ni Mayahudi na wale wote wenye tabia ya Kiyahudi. Miongoni mwa tabia za Kiyahudi ni:

- ☞ Kufanyia Qur'an kejeli.
- ☞ Kuvunja amri za Allah (s.w) zilizo wazi kama walivyovunja amri ya kutofanya kazi siku ya Jumamosi.
- ☞ Kuchanganya haki na batili.
- ☞ Kuchagua kutii baadhi ya amri za Allah (s.w) na kuasi baadhi ya nyingine.
- ☞ Kuacha kuamrisha mema na kukataza maovu

(c) Kujiepusha na mwenendo wa wale waliopotea kabisa. Hawa ni Wakristo ambao waliacha dini ya Uislamu waliyofundishwa na Nabii Issa (a.s). Walibuni Ukristo wenye itikadi ya kumshirikisha Allah (s.w) kwa:

- ☞ Kudai na kuamini kuwa Nabii Issa ni Mwana wa Mungu.
- ☞ Kuitakidi kuwa Allah (s.w) ana nafsi tatu – Mungu Baba, Mungu Mwana na Roho Mtakatifu.
- ☞ Kumfanya Mariam, mama yake Issa kuwa Mama wa Mungu.
- ☞ Kumfanya Nabii Issa Mungu Mtu.

ina aya 6 — **Suuratun Naas 114** — Makka

| | |
|---|---|
| *Kwa jina la Allah mwingi wa Rehma mwenye kurehemu.* | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 1. Sema, Najikinga kwa Bwana mlezi wa watu. | قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ ﴿١﴾ |
| 2. Mfalme wa watu. | مَلِكِ النَّاسِ ﴿٢﴾ |
| 3. Muabudiwa wa Watu. | إِلَٰهِ النَّاسِ ﴿٣﴾ |
| 4. Na shari ya mwenye kutia wasiwasi, mwenye kurejea nyuma. | مِنْ شَرِّ الْوَسْوَاسِ الْخَنَّاسِ ﴿٤﴾ |
| 5. Atiaye wasiwasi nyoyoni mwa watu. | الَّذِي يُوَسْوِسُ فِي صُدُورِ النَّاسِ ﴿٥﴾ |
| 6. Ambaye ni katika majini na watu. | مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ ﴿٦﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Nnaas**

Sura hii inatufundisha kuwa tumuombe Allah (s.w) atukinge na wale wanaoshawishi watu kumuasi Allah (s.w). Ambao huzishawishi nyoyo za watu zielekee kwenye maovu aliyoyakataza Allah (s.w) na kujitenga na mambo mema aliyoyaamrisha Allah (s.w).

Pia sura hii inatutahadharisha kuwa wanaofanya kazi ya kuwashawishi watu kufanya maovu na kuacha kufanya mema ni miongoni mwa majini na watu. Hivyo kwa mujibu wa sura hii, jinni au mtu anayeshawishi watu kufanya maovu huitwa Shetani. Shetani ni adui yetu aliyedhahiri kama Allah (s.w) anavyotufahamisha:

إِنَّ ٱلشَّيْطَٰنَ لَكُمْ عَدُوٌّ فَٱتَّخِذُوهُ عَدُوًّا ۚ إِنَّمَا يَدْعُوا۟ حِزْبَهُۥ
لِيَكُونُوا۟ مِنْ أَصْحَٰبِ ٱلسَّعِيرِ ٦

*Kwa yakini Shetani ni adui yenu. Basi mfanyeni adui (yenu, hivyo msimtii) kwani analiita kundi lake liwe katika watu wa motoni. (35:6)*

Tujiepushe na Sheitani kwa kujitahidi kufanya mema na kujiepusha na maovu. Kila moyo unapotaka kushawishika kuelekea kwenye maovu tujikinge kwa Allah (s.w) kwa kusoma sura hii. Pia tunaweza kujikinga na vishawishi vya Shetani kwa dua ifuatayo:

وَقُل رَّبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ هَمَزَٰتِ ٱلشَّيَٰطِينِ ٩٧

*Na sema Mola wangu Najikinga kwako (uniepushe) na wasiwasi wa mashetani. (23:97)*

ina aya 5 | **Suuratul falaq 113** | Makka

*Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma mwenye kurehemu.*

بسم الله الرحمن الرحيم

1. Sema Najikinga kwa Mola wa Ulimwengu wote.

قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلْفَلَقِ ١

2. Na shari ya alivyoviumba.

مِن شَرِّ مَا خَلَقَ ٢

| | |
|---|---|
| 3.Na shari ya giza la Usiku liingiapo. | وَمِن شَرِّ غَاسِقٍ إِذَا وَقَبَ ٣ |
| 4.Na shari ya wale wanaopuliza mafundoni. | وَمِن شَرِّ النَّفَّٰثَٰتِ فِي الْعُقَدِ ٤ |
| 5.Na shari ya hasidi anapohusudu. | وَمِن شَرِّ حَاسِدٍ إِذَا حَسَدَ ٥ |

**Ujumbe wa Suratul Falaq**

Sura hii inatufahamisha kuwa katika viumbe vya Allah (s.w) kuna vile vyenye kuleta madhara kwa binaadamu. Viumbe hivi vinavyomdhuru mwanaadamu vinaweza kuwa vile vinavyoonekana kwa uwazi kama vile simba, chui n.k. au vile visivyoonekana kwa uwazi kama vile majini, wachawi, mahasidi n.k. Viumbe hawa wanaomdhuru mwanaadamu wakati mwingine waweza kujificha katika giza la usiku au katika pori nene au penginepo.

Tunajifunza katika sura hii kuwa Waislamu tunahimizwa tumuombe Allah (s.w) atukinge na shari ya viumbe vyote vyenye kutudhuru. Kwa kuwa ni viumbe vyake tuna hakika kuwa ni yeye pekee mwenye uwezo wa kutulinda na shari zao. Hivyo Muislamu anapohisi kufikwa na dhara kutokana na kiumbe yeyote anayemuona au asiyemuona, hana budi kutaka ulinzi wa Allah (s.w) kwa kusoma sura hii.

ina aya 4 — **Suuratul Ikhlas 112** — Makka

| | |
|---|---|
| *Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu.* | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 1.Sema: Yeye ni Allah mmoja (tu). | قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ ١ |
| 2.Allah tu ndiye anayestahiki kukusudiwa. | اللَّهُ الصَّمَدُ ٢ |
| 3.Hakuzaa wala hakuzaliwa. | لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ٣ |
| 4.Wala hana anayefafanana naye hata mmoja. | وَلَمْ يَكُن لَّهُ كُفُوًا أَحَدٌ ٤ |

**Ujumbe wa Suratul-Ikhlas**

Sura hii inafundisha kuwa Allah (s.w) ni Mpweke, yaani hana yeyote anayeshirikiana naye katika Uungu wake. Ni yeye pekee aliyeumba viumbe vyote na ndiye pekee anayevimiliki. Hivyo ni yeye pekee anayestahiki kutiiwa, kuogopwa na kutegemewa na kila kiumbe.

Pia sura hii inatufahamisha kuwa Allah (s.w) hakupatikana kwa kuzaliwa au kuumbwa na yeyote, wala hana sifa ya kuzaa wala kuzaliwa. Hivyo Allah (s.w) hawezi kuwa na mtoto. Bali yeye mwenyewe ndiye mwanzo na ndiye mwisho. Yaani muda wote amekuwepo na ataendelea kuwepo milele. Yeye ndiye chanzo cha kila kitu na ndiye anayemiliki mwisho wa kila kitu. Sura hii inatufundisha kuwa Allah (s.w) hafanani na chochote katika viumbe vyake. Yaani Yeye hana mfano.

*ina aya* 5 **Suuratul Lahab 111** *Makka*

| | |
|---|---|
| *Kwa Jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu.* | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 1.Pana kuangamia mikono miwili ya Abu-Lahab! Naye ameshakwisha angamia. | تَبَّتْ يَدَآ أَبِى لَهَبٍ وَتَبَّ ﴿١﴾ |
| 2.Hayatamfaa mali yake wala alivyovichuma. | مَآ أَغْنَىٰ عَنْهُ مَالُهُۥ وَمَا كَسَبَ ﴿٢﴾ |
| 3.(Atakapokufa) atauingia moto wenye mwako (mkubwa kabisa). | سَيَصْلَىٰ نَارًا ذَاتَ لَهَبٍ ﴿٣﴾ |
| 4.Na mkewe mchukuzi wa kuni (za fitina, fatani anayefitinisha watu wasiingie katika dini naye ataingia katika moto huo). | وَٱمْرَأَتُهُۥ حَمَّالَةَ ٱلْحَطَبِ ﴿٤﴾ |
| 5.(Kana kwamba) shingoni mwake iko kamba iliyosokotwa (anayechukulia kuni hizo za fitina. | فِى جِيدِهَا حَبْلٌ مِّن مَّسَدٍۭ ﴿٥﴾ |

## Ujumbe wa Suratul-Lahab

Sura hii imeshuka Makka wakati Mtume (s.a.w) alipoanza kulingania bayana Uislamu katika mwaka wa tatu hivi baada ya kupewa Utume. Aliwaita Maquraish wote na kuwafahamisha kuwa yeye ni Mtume wa Allah (s.w) na kuwa ili waokoke na adhabu ya Allah (s.w) hawana budi kushuhudia kuwa *"Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah"*.

Kitendo hiki cha kuwaita na kuwataka watu wake wasilimu kiliwachukiza sana viongozi wa Kiquraish. Ndipo baba yake mkubwa (Ami yake) aliyeitwa Abu lahab alipomwapiza Mtume kwa kumwambia, "imeangamia mikono yako miwili siku ya leo". Allah (s.w) alishusha sura hii kuwa atakayeangamia ni Abu-Lahab na mkewe kutokana na uadui wao mkubwa dhidi ya Uislamu.

Sura hii inatufundisha kuwa yeyote yule atakayesimama kidete kuupiga vita Uislamu na Waislamu kwa jeuri na kibri hataweza kuuhilikisha Uislamu na Waislamu bali mwishowe ndiye atayehiliki kama ilivyotokea kwa Abu-Lahab na mkewe. Abu-Lahab alikufa bila kusilimu (kafiri) na alikufa kifo cha kudhalilisha kutokana na ugonjwa mbaya wa ngozi uliompelekea kuoza na kunuka yungali hai. Watoto wake na mali yake, havikuweza kumsaidia chochote. Pia mkewe alifariki kafiri na wote wataingia motoni Jahanamu.

Pia sura hii inatufundisha kuwa tusikatishwe tamaa na akina Abu-Lahab wa sasa. Bali tusimame imara katika kuutangaza Uislamu kwa watu wote.

ina aya 3 — **Suuratun Nasr 110** — Madina

| | |
|---|---|
| *Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu.* | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 1. Itakapofika nusura ya Allah (s.w) na kushinda. | إِذَا جَآءَ نَصْرُ ٱللَّهِ وَٱلْفَتْحُ ۝١ |
| 2. Na utakapowaona watu wakiingia katika dini ya Allah makundi makundi. | وَرَأَيْتَ ٱلنَّاسَ يَدْخُلُونَ فِى دِينِ ٱللَّهِ أَفْوَاجًا ۝٢ |
| 3. Basi hapo mtakase Mola wako pamoja na kumsifu, Umuombe msamaha, hakika yeye ndiye apokeaye toba. | فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَٱسْتَغْفِرْهُ ۚ إِنَّهُۥ كَانَ تَوَّابًۢا ۝٣ |

**Ujumbe wa Surat-Nasr**

Sura hii inampa Mtume (s.a.w) bishara kuwa itakapofika nusura na kupata ushindi dhidi ya maadui wa Uislamu, na watu wakawa wanaingia Uislamu makundi kwa makundi ajue kuwa amekamilisha kazi yake na ajiandae kurejea kwa Mola wake kwa kumtukuza na kumsifu pamoja na kumuomba maghufira Kutokana na sura hii tunajifunza kuwa:

(i) Nusra na ushindi hutoka kwa Allah (s.w). Allah (s.w) amewaahidi Waislamu kuwa watakapojitahidi kupigania dini yake kwa kadiri ya uwezo wao kwa kutoa mali zao na nafsi zao, atawanusuru na kuwapa ushindi mkubwa hapa hapa duniani.

(ii) Waislamu baada ya kupata nusra na ushindi, hatupaswi kujisikia na kujivuna na kufanya kibri na uharibifu bali tunatakiwa tumshukuru Allah (s.w) kwa kumtakasa pamoja na kumuomba msamaha kwa makosa yetu ili tuwe safi mbele yake.

(iii) Kwa Waislamu mafanikio halisi si kuwa na wingi wa mali au vyeo vikubwa bali mafanikio halisi hupatikana kwa kusimama dini ya Allah (s.w).

## ina aya 6 — Suuratul Kaafiruuna 109 — Makka

| | |
|---|---|
| *Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma mwenye kurehemu.* | بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ |
| 1. Sema, Enyi makafiri. | قُلْ يَٰٓأَيُّهَا ٱلْكَٰفِرُونَ ﴿١﴾ |
| 2. Siabudu mnachoabudu. | لَآ أَعْبُدُ مَا تَعْبُدُونَ ﴿٢﴾ |
| 3. Wala nyinyi hamumuabudu ninayemuabudu. | وَلَآ أَنتُمْ عَٰبِدُونَ مَآ أَعْبُدُ ﴿٣﴾ |
| 4. Wala sitaabudu mnachoabudu. | وَلَآ أَنَا۠ عَابِدٌ مَّا عَبَدتُّمْ ﴿٤﴾ |
| 5. Wala nyinyi hamtaabudu ninayemuabudu. | وَلَآ أَنتُمْ عَٰبِدُونَ مَآ أَعْبُدُ ﴿٥﴾ |
| 6. Nyinyi mna dini yenu nami nina dini yangu. | لَكُمْ دِينُكُمْ وَلِىَ دِينِ ﴿٦﴾ |

## Ujumbe wa Suratul Kaafiruun

Mwanzoni mwa Utume wa Muhammad (s.a.w) makafiri wa Makka walikamia kuzuia Uislamu usienee. Walitumia mbinu mbali mbali ili kufikia lengo lao hili. Mbinu mojawapo waliyoitumia ni ile ya kutaka kufanya makubaliano na Mtume (s.a.w) juu ya kuabudu (Ibada). Ujumbe wa makafiri wa Kiquraish ulipeleka mswada wa makubaliano kwa Mtume (s.a.w) pamoja na Waislamu wajiunge na makafiri katika kuabudu masanamu kwa kipindi cha mwaka mmoja. Kisha mwaka unaofuatia makafiri hao watashiriki na Waislamu katika kumuabudu Allah (s.w). Waendelee kushirikiana hivyo hivyo ili pawe na ushirikiano na mshikamano baina ya kabila la Kiquraish na taifa la Waarabu kwa ujumla. Allah (s.w) alimshushia Wahay Mtume wake kuwa awajibu kwa kuwasomea sura hii. Kutokana na sura hii tunajifunza kuwa:

(i) Kila mwanaadamu anafuata dini moja au nyingine. Hakuna mtu asiye na dini.Ukafiri nao ni dini.

(ii) Uislamu ni dini ya Allah (s.w) isiyohusiana wala kukubaliana na dini yoyote ile. Hivyo Muislamu wa kweli hana budi kuufuata Uislamu wote kama ulivyoelekezwa na Allah (s.w) na Mtume wake.

(iii) Waislamu wa kweli ni wale wasiochanganya haki na batili kwa kuwahofia makafiri. Waislamu wana utaratibu wao wa maisha na makafiri wana utaratibu wao. Daima Waislamu wa kweli hawawezi kushikamana na makafiri katika kuendesha maisha yao ya kila siku.

## *ina aya 3* — Suuratul Kawthar 108 — *Makka*

| | |
|---|---|
| *Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye kurehemu.* | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 1. Hakika tumekupa kheri nyingi. | إِنَّا أَعْطَيْنَاكَ الْكَوْثَرَ ﴿١﴾ |
| 2. Basi Swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili yake). | فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَانْحَرْ ﴿٢﴾ |
| 3. Hakika adui yako ndiye atakayekuwa mkiwa (atakatikiwa na kila la kheri). | إِنَّ شَانِئَكَ هُوَ الْأَبْتَرُ ﴿٣﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Kawthar**

Makafiri wa Makka walitumia mbinu mbali mbali ili kuuzuia Uislamu usifike kwa watu. Mbinu mojawapo ni ile ya kuwakatisha tamaa na kumvunja moyo Mtume kwa kumwita Abtar, aliyekatikiwa na kheri. Walimuita Mtume Abtar baada ya kufiwa na mtoto wake pekee wa kiume aliyeitwa Kassim na baada ya kuacha shughuli za biashara na kuondokewa na utajiri wa mali aliokuwa nao baada ya kuoana na Khadija.

Kwa uoni wa makafiri, mtu wa maana na mweye hadhi ni yule mwenye mali nyingi na watoto wengi wa kiume. Na mtu asiye na vitu hivi huonekana kuwa amekatikiwa na kheri. Kwa chuki zao dhidi ya Mtume na Uislamu, viongozi wa makafiri kama vile akina Abu Jahal, Walid bin Al-Mughira na Abu-Lahab waliamua kumdhihaki Mtume wa Allah (s.w) kwa kuwatangazia watu kuwa Mtume Muhammad ni Abtar.

Allah (s.w) alimliwaza Mtume wake na Waislamu kuwa Mtume hajakatikiwa na kheri, bali kinyume chake amepewa kheri nyingi ikiwa ni pamoja na:

(i) Kupewa Utume na kuletewa Wahay kila wakati akifahamishwa mambo makubwa na matukufu kutoka kwa Allah (s.w).

(ii) Kupewa hadhi ya kuwa Mtume wa walimwengu wote na Rehema kwa viumbe vyote.

(iii) Kupewa hadhi ya kuwa Mtume wa mwisho aliyekamilisha ujumbe wa Allah (s.w) na kushushiwa Qur-an, kitabu cha mwisho cha Allah (s.w) ambacho amekihifadhi mpaka siku ya mwisho.

(iv) Vile vile Mtume (s.a.w) ameahidiwa kupata cheo kikubwa huko akhera kuliko yeyote yule. Vile vile siku ya Kiyama ameahidiwa kupewa nafasi ya kwanza ya kuwashufaia watu wote ikiwa ni pamoja na Mitume wote wa Allah (s.w)

Kutokana na sura hii tunajifunza kuwa:

(i) Kwa mtazamo wa Uislamu mafanikio hayapimwi kwa wingi wa mali na watoto bali hupimwa kwa kuridhiwa na Allah (s.w).

(ii) Hakuna neema kubwa aliyotunukiwa Muislamu, kuliko kuujua Uislamu, kuufuata vilivyo na kuusimamisha katika jamii.

(iii) Waislamu daima wasikatishwe tamaa na kauli mbali mbali za makafiri bali wanatakiwa wasubiri na wazidi kutekeleza wajibu wao kama walivyoamrishwa na Mola wao.

(iv) Hatima ya maadui na wapinzani wa Uislamu ni kuhasirika na kuhiliki. Kwa upande mwingine, kila kukicha Waislamu watazidi kuendea mafanikio iwapo watakuwa imara katika kupigania dini ya Allah (s.w).

ina aya 7 — **Suuratul Maun 107** — Makka

*Kwa jina la Allah (s.w) Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu.*

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

1. Je Unamjua yule anayekadhibisha dini (asiyeamini malipo ya Akhera)?

أَرَءَيْتَ الَّذِي يُكَذِّبُ بِالدِّينِ ﴿١﴾

2. Huyu ni yule anayemsukuma yatima.

فَذَٰلِكَ الَّذِي يَدُعُّ الْيَتِيمَ ﴿٢﴾

3. Wala hajihimizi (yeye wala wengine) kuwalisha maskini.

وَلَا يَحُضُّ عَلَىٰ طَعَامِ الْمِسْكِينِ ﴿٣﴾

4. Basi adhabu itawathubutikia wanaoswali.

فَوَيْلٌ لِّلْمُصَلِّينَ ﴿٤﴾

5. Ambao wanapuuza swala zao.

الَّذِينَ هُمْ عَن صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ ﴿٥﴾

6. Ambao hufanya riyaa.

الَّذِينَ هُمْ يُرَاءُونَ ﴿٦﴾

7. Nao hunyima misaada midogo midogo.

وَيَمْنَعُونَ الْمَاعُونَ ﴿٧﴾

**Ujumbe wa Suratul-Maun**

Muumini wa kweli ni yule mwenye yakini kuwa kuna maisha ya akhera ambapo kila mtu atalipwa kulingana na amali zake alizozifanya hapa ulimwenguni. Wale waliojitahidi kufanya mema kwa ajili ya Allah (s.w) na wakajitahidi kujiepusha na maovu watalipwa Pepo. Pepo ni mahali pazuri sana pa kushukia mtu.

Ama wale waliopuuza na kufanya yale yote aliyoyakataza Allah (s.w) wataadhibiwa motoni. Motoni ni marejeo mabaya sana kwa mtu.

Muumini wa kweli hatapuuza kufanya jambo lolote la kheri au kujiepusha na jambo lolote la shari. Kwani katika sura hii tunajifunza kuwa mtu atakuwa amekadhibisha siku ya malipo (maisha ya akhera), hata kama anadai kuwa ni Muislamu iwapo atakuwa ni mwenye kufanya yafuatayo:

(i) Anawadhulumu au kuwanyanyasa yatima.

(ii) Hasaidii masikini na wengineo wanaohitajia msaada na huku akiwa ana uwezo wa kutoa msaada huo, wala hawahimizi wengine kutoa msaada.

(iii) Hajali matatizo ya wenziwe.

(iv) Anapuuza swala kwa kutoziswali kwa kuzingatia sharti na nguzo zake. Huswali atakavyo yeye bila ya kuzingatia maelekezo ya Allah (s.w) na Mtume wake.

(v) Hufanya mambo mema kwa ajili ya kuwapendezesha watu na si kwa ajili ya kupata radhi za Allah (s.w).

(vi) Ni mchoyo wa kutoa hata misaada midogo midogo ambayo anauwezo nayo.

Kinyume chake, anayeamini siku ya malipo hufanya kama tunavyoelekezwa katika aya zifuatazo:

وَيُطْعِمُونَ ٱلطَّعَامَ عَلَىٰ حُبِّهِۦ مِسْكِينًا وَيَتِيمًا وَأَسِيرًا ﴿٨﴾
إِنَّمَا نُطْعِمُكُمْ لِوَجْهِ ٱللَّهِ لَا نُرِيدُ مِنكُمْ جَزَآءً وَلَا شُكُورًا ﴿٩﴾ إِنَّا
نَخَافُ مِن رَّبِّنَا يَوْمًا عَبُوسًا قَمْطَرِيرًا ﴿١٠﴾ فَوَقَىٰهُمُ ٱللَّهُ شَرَّ ذَٰلِكَ
ٱلْيَوْمِ وَلَقَّىٰهُمْ نَضْرَةً وَسُرُورًا ﴿١١﴾

*Na huwalisha chakula masikini na yatima na wafungwa hali ya kuwa wenyewe wana kipenda (chakula hicho: Husema wenyewe katika nyoyo zao wanapowapa chakula hicho). Tunakulisheni kwa ajili ya kutaka radhi kwa Allah, hatutaki kwenu malipo wala shukurani. Hakika sisi tunaiogopa kwa Mola wetu hiyo siku yenye shida na taabu. Basi Allah atawalinda na shari ya siku hiyo na kuwakutanisha na neema na furaha. (76:8-11)*

Hivyo tunajifunza kutokana na sura hii kuwa ili tuwe waumini wa kweli hatuna budi kufanya yafuatayo:

(i) Kusimamisha swala kama ilivyoelekezwa katika Qur-an na Sunnah.

(ii) Kujitahidi kuwa wakarimu na kuwafanyia watu wema kwa kadiri ya uwezo wetu kwa matarajio ya kupata radhi za Allah (s.w).

(iii) Kuepuka uchoyo, kuwadhulumu watu haki zao na kuwafanyia maovu wengine.

(iv) Kufanya kila jambo kwa ikhlas kwa kutarajia kupata radhi za Allah (s.w).

ina aya 4 — **Suuratul Quraysh 106** — Makka

*Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma, Mwenye Kurehemu.*

بسم الله الرحمن الرحيم

1. Ili kuwafanya Makurayshi waendelee.

لِإِيلَٰفِ قُرَيْشٍ ①

2. Waendelee na safari zao za wakati wa kusi (kwenda Yaman) na wakati wa kaskazi (kwenda Shamu) ndiyo maana tukajaalia jeshi la ndovu kushindwa).

إِۦلَٰفِهِمْ رِحْلَةَ ٱلشِّتَآءِ وَٱلصَّيْفِ ②

3. Basi nawamuabudu Bwana wa nyumba hii (Al-Kaaba).

فَلْيَعْبُدُوا۟ رَبَّ هَٰذَا ٱلْبَيْتِ ③

5. Ambaye anawalisha (wakati Waarabu wenziwao wamo) katika njaa, na anawapa amani (wakati wenziwao wamo) katika khofu.

ٱلَّذِىٓ أَطْعَمَهُم مِّن جُوعٍ وَءَامَنَهُم مِّنْ خَوْفٍۭ ④

**Ujumbe wa Suratul-Quraysh**

Quraysh ni kabila la Mtume Muhammad (s.a.w). Hata kabla ya kuzaliwa Mtume Muhammad (s.a.w) kabila la Quraysh lilikuwa tukufu na kuheshimiwa sana na makabila yote mengine ya Bara Arabu kutokana na nafasi yake ya kuitunza na

kuilinda Ka'aba. Ka'aba ni nyumba ya awali ya Allah (s.w) iliyojengwa kwa ajili ya kumuabudu.Tunafahamishwa katika Qur-an

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِى بِبَكَّةَ مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَٰلَمِينَ ﴿٩٦﴾

*Kwa yakini nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu ni ile iliyopo Makka, yenye baraka na uongozi kwa ajili ya walimwengu wote. (3:96)*

Bila shaka nyumba hii atakuwa ameijenga Nabii Adamu na watoto wake. Baada ya muda mrefu kupita nyumba hii ilichakaa na kubakia msingi tu. Kisha Nabii Ibrahimu na mwanawe Nabii Ismail walipewa amri na Mola wao ya kuijenga Ka'aba upya juu ya msingi ule ule wa asili kama tunavyofahamishwa katika Qur-an:

وَإِذْ يَرْفَعُ إِبْرَٰهِۦمُ ٱلْقَوَاعِدَ مِنَ ٱلْبَيْتِ وَإِسْمَٰعِيلُ رَبَّنَا تَقَبَّلْ مِنَّآ ۖ إِنَّكَ أَنتَ ٱلسَّمِيعُ ٱلْعَلِيمُ ﴿١٢٧﴾

*Na (kumbukeni habari hii pia): Ibrahim alipoinua kuta za nyumba (hii ya Ka'aba) na Ismail (kisha wakaomba wakasema): Ee Mola wetu! Tukubalie (amali yetu hii ya kujenga Ka'aba) Hakika wewe ndiye Mwenye kujua Mwenye kusikia. (2:127)*

Katika sura hii Maquraysh wanakumbushwa kuwa kilichowafanya waheshimiwe na kutukuzwa na makabila mengine kiasi cha kutoshambuliwa na kubughudhiwa katika biashara zao ni Ka'aba, nyumba ya Allah (s.w). Hivyo wanahimizwa washukuru neema hii ya kuwa na amani na shibe wakati wenzao wako katika khofu na njaa. Washukuru neema hii kwa kumuabudu Bwana wa Ka'aba inavyostahiki. Kutokana na sura hii tunajifunza yafuatayo:

(i) Neema zote tulizo nazo ametupa Allah (s.w).Hivyo hatuna budi kushukuru neema hizi kwa kumuabudu Allah (s.w) ipasavyo.

(ii) Neema kubwa kuliko zote ni kuwa Muislamu. Uislamu ni dini ya Bwana wa Ka'aba yenye kuleta amani na furaha katika maisha ya jamii endapo itafuatwa vilivyo. Hatuna budi kushukuru neema hii kwa kumuabudu Allah (s.w) inavyostahiki katika maisha yetu yote.

ina aya 5 | **Suuratul Fyil** | Makka

| | |
|---|---|
| *Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu.* | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 1.Je! Huoni jinsi Mola wako alivyowafanya watu wenye ndovu? | أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَابِ الْفِيلِ ﴿١﴾ |
| 2.Je! Hakujaalia vitimbi vyao kuharibika. | أَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ فِي تَضْلِيلٍ ﴿٢﴾ |
| 3.Na akawapelekea ndege makundi kwa makundi. | وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ﴿٣﴾ |
| 4.Wakawapiga kwa mawe ya udongo wa kuchoma. | تَرْمِيهِم بِحِجَارَةٍ مِّن سِجِّيلٍ ﴿٤﴾ |
| 5.Akawafanya kama majani yaliyoliwa. | فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍ ﴿٥﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Fyl**

Sura hii inatukumbusha juu ya kuangamizwa kwa jeshi la tembo. Tukio lililotokea Makka miezi michache kabla ya kuzaliwa Mtume Muhammad (s.a.w).

Katika mwaka wa 570 A.D. Abraha al-Ashram aliyekuwa Gavana wa Yemen chini ya ufalme wa Kikristo wa Uhabeshi, aliandaa jeshi kwa nia ya kuibomoa Ka'aba ili kuwazuia watu wasiende kuhiji Makka badala yake waende Yemen.

Awali alijenga Kanisa kubwa na zuri ili watu wavutiwe kwenda kufanya hija huko. Lakini Watu hawakukubali kuacha mila ya Nabii Ibrahim na Nabii Ismail. Hata Waarabu wa Yemen waliendelea kwenda kuizuru Ka'aba wakati wa hija na kuliacha Kanisa Yemen.

Abraha alishikwa na husuda na chuki. Akaamua kuandaa jeshi kubwa lililotumia tembo kama vipando kwa lengo la kwenda kuivunja Ka'aba.

Maquraysh, walinzi wa Ka'aba hawakuwa na uwezo wa kuihami Ka'aba. Abd-Al-Muttalib, babu yake Mtume (s.a.w) ndiye aliyekuwa kiongozi wa Makka wakati huo. Kwa niaba ya Maquraysh, Abd Al-Muttalib, aliingia ndani ya Ka'aba na kumuomba mwenye Ka'aba ailinde nyumba yake. Kisha akawaamuru watu wake waondoke na familia zao ili kumwachia Abraha atimize azma yake bila ya upinzani wowote.

Kabla ya jeshi la Abraha halijafika Makka, Allah (s.w) mwenye Ka'aba alileta jeshi la ndege wadogo wadogo wanaoitwa Ababil. Ndege hawa walibeba silaha ya vijiwe vya udongo uliochomwa na kuliangamiza jeshi zima la watu wa tembo pamoja na Abraha mwenyewe. Kutokana na sura hii tunapata mafunzo yafuatayo:

(i) Allah (s.w) yupo na ndiye Bwana wa Ka'aba.

(ii) Hakuna nguvu inayomshinda Allah (s.w) hata kama nguvu hiyo ni kubwa kiasi gani.

(iii) Kila kiumbe katika mbingu na ardhi kinaweza kuwa jeshi la Allah (s.w).

(iv) Wenye azma ya kuivunja dini ya Allah (s.w) daima watakuwa ni wenye kushindwa na kuhiliki.

(v) Nusra na masaada wa Allah (s.w) utapatikana wakati wowote kwa wale wenye kupigania dini yake na kumtegemea yeye tu basi.

## ina aya 9 — Suuratul Humazah 104 — Makka

*Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu.*

بسم الله الرحمن الرحيم

1. Adhabu kali itamdhibitikia kila mwenye kuramba kisogo, msengenyaji.

وَيْلٌ لِّكُلِّ هُمَزَةٍ لُّمَزَةٍ ﴿١﴾

2. Ambaye amekusanya mali na kuyahesabu.

الَّذِي جَمَعَ مَالًا وَعَدَّدَهُ ﴿٢﴾

3. Anadhani ya kuwa mali yake yatamdumisha milele.

يَحْسَبُ أَنَّ مَالَهُ أَخْلَدَهُ ﴿٣﴾

| | |
|---|---|
| 4.Hasha! Bila shaka atavurumizwa katika (moto unaoitwa) Hutama. | كَلَّا لَيُنۢبَذَنَّ فِى ٱلْحُطَمَةِ ﴿٤﴾ |
| 5.Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ukajua) ni nini Hutama? | وَمَآ أَدْرَىٰكَ مَا ٱلْحُطَمَةُ ﴿٥﴾ |
| 6.(Huo) ni moto wa Allah uliowashwa (kwa ukali barabara). | نَارُ ٱللَّهِ ٱلْمُوقَدَةُ ﴿٦﴾ |
| 7.Ambao unapanda nyoyoni. | ٱلَّتِى تَطَّلِعُ عَلَى ٱلْأَفْـِٔدَةِ ﴿٧﴾ |
| 8.Hakika huo (moto) watafungiwa (wawemo ndani yake). | إِنَّهَا عَلَيْهِم مُّؤْصَدَةٌ ﴿٨﴾ |
| 9.Katika magogo marefu marefu. | فِى عَمَدٍ مُّمَدَّدَةٍۭ ﴿٩﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Humazah**

Sura hii inaashiria adhabu kali ya kuingizwa kwenye moto mkali sana uitwao Hutama kwa wale wenye kusengenya na wenye kulimbikiza mali bila ya kuyatolea Zakat na sadakat.

Kusengenya ni kumzungumza kwa ubaya mtu asiyekuwepo. Pia inahesabika kuwa mtu amesengenya kwa kutumia ishara kama vile kumng'ong'a mtu au kumramba kisogo au kumuonyesha kwa ulimi na huku mwenyewe akiwa hana habari kuwa anaashiriwa. Katika Qur-an ubaya wa kusengenya unafananishwa na mtu kula nyama ya maiti ya ndugu yake:

وَلَا يَغْتَب بَّعْضُكُم بَعْضًا ۚ أَيُحِبُّ أَحَدُكُمْ أَن يَأْكُلَ
لَحْمَ أَخِيهِ مَيْتًا فَكَرِهْتُمُوهُ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ تَوَّابٌ رَّحِيمٌ ﴿١٢﴾

*Wala baadhi yenu wasiwasengenye wengine. Je! Mmoja wenu anapenda kula nyama ya nduguye aliyekufa? La, hapendi. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba, mwingi wa kurehemu. (49:12)*

Muislamu wa kweli hana budi kujiepusha mbali na kusengenya. Tunafahamishwa katika Qur-an kuwa katika mali ya tajiri kuna haki za maskini, fukara, yatima, walemavu na wenye kufikiwa na matatizo mbali mbali kama vile kuharibikiwa safarini, kukumbwa na mafuriko, kuunguliwa nyumba na kadhalika.

Hivyo tajiri atakapojizuilia kutoa mali yake kwa njia ya Zakat atakuwa amewadhulumu na atastahiki kupata adhabu kali ya moto wa Hutama.

Pia katika Qur-an tunafahamishwa:

وَٱلَّذِينَ يَكْنِزُونَ ٱلذَّهَبَ وَٱلْفِضَّةَ وَلَا يُنفِقُونَهَا
فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ فَبَشِّرْهُم بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ٣٤

*Na wale wakusanyao dhahabu na fedha wala hawazitoi katika njia ya Mwenyezi Mungu, wape habari ya adhabu inayoumiza. (9:34)*

## ina aya 3 — Suuratul Asr 103 — Makka

بسم الله الرحمن الرحيم

*Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu.*

وَٱلْعَصْرِ ١

1. Naapa kwa zama.

إِنَّ ٱلْإِنسَٰنَ لَفِى خُسْرٍ ٢

2. Kuwa binaadamu yumo katika hasara.

إِلَّا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ وَتَوَاصَوْا۟ بِٱلْحَقِّ وَتَوَاصَوْا۟ بِٱلصَّبْرِ ٣

3. Isipokuwa wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri, na wakausiana haki na wakausiana (kushikamana) na subira.

## Ujumbe wa Suratul-'Asr

Katika sura hii Allah (s.w) anaapa kwa kutumia wakati ('asr) kuwa wanaadamu wote wako katika hasara ila wale wenye kutekeleza yafuatayo yote kwa pamoja:

(i) Kuamini.

(ii) Kufanya amali njema.

(iii) Kuusiana haki.

(iv) Kuusiana subira.

**Kuamini**

Wanaadamu wenye akili timamu wanapaswa wawe na yakini juu ya vipengele vyote vya nguzo za Imani. Yaani wanapaswa wamuamini Allah (s.w), Malaika wake, Vitabu vyake, Mitume wake, Siku ya Mwisho na Qadar yake.

**Kutenda amali njema**

Amali njema ni matendo yote mema anayoyaridhia Allah (s.w) na Mitume wake. Muumini wa kweli ni yule anayeishi katika maisha yake yote kwa kufuata maelekezo ya Allah (s.w) yanayopatikana katika vitabu vyake na maelekezo ya Mitume tunayopata katika Hadithi sahihi.

**Kuusia haki**

Kuusiana haki ni kuwalingania watu juu ya Uislamu. Muumini wa kweli pamoja na yeye mwenyewe kutekeleza Uislamu vilivyo katika maisha yake yote, analazimika kuwalingania watu katika jamii wafuate Uislamu.

**Kuusia Subira**

Kuusia subira ni kuwausia watu wasubiri katika

(i) Kufanya amali njema. Yaani waendelee kufanya mema bila ya kuchoka au kukata tamaa mpaka watakapokutana na Mola wao.

(ii) Kujiepusha na mambo maovu japo yanaonekana yenye kupendeza machoni mwa watu au katika nafsi ya mtu. Yaani kuendelea kuacha maovu aliyoyakataza Allah (s.w) na Mtume wake bila ya kuchoka mpaka mwisho wa maisha yake.

(iii) Kuvumilia matatizo mbali mbali yanayowafika watu kama vile kufiwa na wapenzi wetu, kuugua au kuuguliwa, kufikwa na umasikini na kadhalika. Kama Qur-an inavyotuusia:

وَلَنَبْلُوَنَّكُم بِشَيْءٍ مِّنَ ٱلْخَوْفِ وَٱلْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ ٱلْأَمْوَٰلِ وَٱلْأَنفُسِ وَٱلثَّمَرَٰتِ ۗ وَبَشِّرِ ٱلصَّـٰبِرِينَ ﴿١٥٥﴾

*Na tutakutieni katika msukosuko wa khofu, njaa, upungufu wa mali, kufiwa na watu na upungufu wa matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri.*

ٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَـٰبَتْهُم مُّصِيبَةٌ قَالُوٓا۟ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيْهِ رَٰجِعُونَ ﴿١٥٦﴾

*Ambao uwapatapo msiba husema: "Hakika sisi ni wa Allah na kwake yeye tutarejea.*

أُو۟لَـٰٓئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَوَٰتٌ مِّن رَّبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ ۖ وَأُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُهْتَدُونَ ﴿١٥٧﴾

*Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na Rehema na ndio wenye kuongoka. (2:155-157)*

(iv)Kuvumilia maudhi yatokanayo na watu tunaoishi pamoja katika maisha yetu ya kila siku. Kwani haitokei watu kuishi pamoja bila ya kutofautiana hapa na pale.

Kutokana na sura hii tunajifunza kuwa ili mwanaadamu aweze kuishi kwa furaha na amani hapa ulimwenguni hana budi kutekeleza kwa pamoja na kwa ukamilifu haya mambo manne ya kuamini vilivyo, kufanya amali njema, kuusia haki na kuusia subira. Pia wenye kutekeleza haya ndio tu pekee watakaostahiki kupata radhi za Allah (s.w) na kustahiki makazi mema ya peponi.

ina aya 8

## Suuratut Takaathur 102

Makka

| | |
|---|---|
| *Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu.* | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 1.Kumekughafilisheni katika kutafuta wingi (wa mali, madaraka na watoto na kadhalika). | أَلْهَاكُمُ التَّكَاثُرُ ﴿١﴾ |
| 2.Hata mumeingia makaburini. | حَتَّىٰ زُرْتُمُ الْمَقَابِرَ ﴿٢﴾ |
| 3.Sivyo, hivyo karibuni hivi mtajua (kuwa sivyo hivyo). | كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٣﴾ |
| 4.Kisha (nasema) sivyo hivyo, karibuni hivi mtajua (kuwa sivyo hivyo). | ثُمَّ كَلَّا سَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿٤﴾ |
| 5.Sivyo hivyo, lau kama (nyinyi) mnajua ujuzi wa yakini (kuwa sivyo hivyo, basi msingefanya hivyo). | كَلَّا لَوْ تَعْلَمُونَ عِلْمَ الْيَقِينِ ﴿٥﴾ |
| 6.Hakika mtauona moto. | لَتَرَوُنَّ الْجَحِيمَ ﴿٦﴾ |
| 7.Kisha (nasema) mtauona kwa yakini. | ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا عَيْنَ الْيَقِينِ ﴿٧﴾ |
| 8.Kisha kwa hakika mtaulizwa siku hiyo juu ya Neema (Mlizopewa mlizitumiaje). | ثُمَّ لَتُسْأَلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ النَّعِيمِ ﴿٨﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Takaathur**

Sura hii inamtahadharisha mwanaadamu kuwa asizame kutafuta wingi wa vitu vya starehe za hapa ulimwenguni mpaka impelekee kusahau lengo la kuumbwa kwake. Lengo la kuumbwa mwanaadamu ni kumuabudu Allah (s.w) kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ٥٦

*Sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu. (51:56)*

Kumuabudu Allah (s.w) ni kumtumikia katika maisha yetu yote kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake yote. Hivyo wakati wa kuchuma na kutafuta mahitajio ya maisha ya hapa ulimwenguni hatuna budi kuchunga mipaka ya Allah (s.w). Hatuna budi kuchuma na kutumia mali kama alivyoagiza Allah (s.w). kinyume na maagizo yake, tujue kuwa tunangojewa na adhabu kali ya moto wa Jahannam.

## Suuratut Qaariah 101

ina aya 8 — Makka

| | |
|---|---|
| *Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu.* | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 1.(Msiba) ugongao nyoyo. | الْقَارِعَةُ ١ |
| 2.(Msiba) ugongao nyoyo ni upi huo? | مَا الْقَارِعَةُ ٢ |
| 3.Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ukaujua) ni upi huo (msiba) ugongao nyoyo? | وَمَا أَدْرَاكَ مَا الْقَارِعَةُ ٣ |
| 4.Siku ambayo watu watakuwa kama madu madu (watoto wa nzige) waliotawanywa. | يَوْمَ يَكُونُ النَّاسُ كَالْفَرَاشِ الْمَبْثُوثِ ٤ |
| 5.Na milima itakuwa kama sufi zilizochanguliwa (zikawa zinapeperuka). | وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ الْمَنفُوشِ ٥ |
| 6.Basi yule mizani yake itakayokuwa nzito. | فَأَمَّا مَن ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ ٦ |

| | |
|---|---|
| 7.Huyo atakuwa katika maisha yanayompendeza. | فَهُوَ فِي عِيشَةٍ رَّاضِيَةٍ ﴿٧﴾ |
| 8.Na yule ambaye mizani yake itakuwa nyepesi. | وَأَمَّا مَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ ﴿٨﴾ |
| 9. Huyo maskani yake yatakuwa katika (huo moto wa) Hawiya. | فَأُمُّهُ هَاوِيَةٌ ﴿٩﴾ |
| 10. Na ni jambo gani litakalokujulisha (hata ukaujua) ni nini huo Hawiya? | وَمَا أَدْرَاكَ مَا هِيَهْ ﴿١٠﴾ |
| 11. Ni moto uwakao kwa ukali (kweli kweli). | نَارٌ حَامِيَةٌ ﴿١١﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Qaari'ah**

Sura hii inatukumbusha juu ya siku ya Kiyama. Inatufahamisha kuwa mazingira ya kiyama yatakuwa magumu sana. Ugumu utazidi kwa makafiri waliokataa kufuata mwongozo wa Allah (s.w) hapa ulimwenguni. Ugumu huu utaendelea mpaka watu watakapofikishwa mbele ya Mola wao tayari kuhukumiwa kulingana na matendo yao hapa ulimwenguni. Watu siku hiyo watagawanyika katika makundi makubwa mawili. Kundi la watu wema na kundi la watu waovu.

Watu wema ni wale ambao katika maisha yao ya hapa ulimwenguni walijitahidi kumtii Allah (s.w) na Mitume wake. Pia walijitahidi kuwafanyia watu wema kwa ajili ya kutafuta radhi za Allah (s.w). Hawa watalipwa malipo mema (thawabu) ambayo yatafanya mizani zao ziwe nzito kwa upande wa wema. Kuelemea mizani kwa upande wa wema ni ishara ya kufaulu na kustahiki malipo ya furaha na amani huko peponi.

Watu waovu ni wale ambao katika maisha yao hapa duniani walikataa mwongozo wa Allah (s.w), badala yake wakaishi watakavyo. Wakazama katika kumuasi Allah (s.w) na Mitume wake. Wakaishi katika kufanya maovu ya namna mbali mbali. Watu hawa watastahiki kulipwa uovu (dhambi) sawa na uovu wao, malipo ambayo yataifanya mizani zao zielemee upande wa uovu. Kuelemea mizani upande wa uovu ni ishara ya kufeli na kustahiki adhabu kali ya moto wa Hawiya.

Sura hii inatufundisha kuwa:

(i) Tujitahidi kufanya amali njema kwa kumtii Allah (s.w) na Mtume wake inavyostahiki ili mizani yetu ipate kuwa nzito katika hiyo siku ya hukumu ili tustahiki kupata pepo.

(ii) Tujitahidi kujiepusha kumuasi Allah (s.w) na Mtume wake ili mizani zetu zisiwe nyepesi upande wa wema na zikawa nzito upande wa maovu katika hiyo siku ya hukumu na tukastahiki kwenda motoni badala ya peponi.

(iii) Pamoja na jitihada hizi tunatakiwa daima tuombe kuepushwa na adhabu ya moto na badala yake tuingizwe peponi kwa kusema:

رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِى ٱلْءَاخِرَةِ
حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ﴿٢٠١﴾

*"Mola wetu! Tupe mema duniani na (tupe) mema akhera na tulinde na adhabu ya moto. (2:201)*

وَٱلَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا ٱصْرِفْ عَنَّا عَذَابَ
جَهَنَّمَ إِنَّ عَذَابَهَا كَانَ غَرَامًا ﴿٦٥﴾

*Mola wetu! Tuondolee adhabu ya Jahannam, bila shaka adhabu yake ni yenye kuendelea.*

إِنَّهَا سَآءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٦٦﴾

*Hakika hiyo (Jahannam) ni kituo kibaya na mahali (pabaya kabisa) pa kukaa. (25:65-66)*

ina aya 11

# Suuratut 'Aadiyaat 100

Madina

| | |
|---|---|
| *Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu.* | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 1.Naapa kwa (farasi) wanaokwenda mbio wakihema. | وَالْعٰدِيٰتِ ضَبْحًا ﴿١﴾ |
| 2.Na wakitoa moto kwa kupiga kwato (zao chini). | فَالْمُوْرِيٰتِ قَدْحًا ﴿٢﴾ |
| 3.Wakashambulia wakati wa asubuhi. | فَالْمُغِيْرٰتِ صُبْحًا ﴿٣﴾ |
| 4.Wakarusha mavumbi (makubwa) wakati huo. | فَاَثَرْنَ بِهٖ نَقْعًا ﴿٤﴾ |
| 5.Wakaingia katika kundi (la maadui wakapigana). | فَوَسَطْنَ بِهٖ جَمْعًا ﴿٥﴾ |
| 6.Bila shaka binaadamu anamkanusha Mola wake. | اِنَّ الْاِنْسَانَ لِرَبِّهٖ لَكَنُوْدٌ ﴿٦﴾ |
| 7.Naye anajua haya. | وَاِنَّهٗ عَلٰى ذٰلِكَ لَشَهِيْدٌ ﴿٧﴾ |
| 8.Na ana mapenzi makubwa kabisa ya kupenda mali. | وَاِنَّهٗ لِحُبِّ الْخَيْرِ لَشَدِيْدٌ ﴿٨﴾ |
| 9.Je, hajui watakapofufuliwa waliomo makaburini. | اَفَلَا يَعْلَمُ اِذَا بُعْثِرَ مَا فِى الْقُبُوْرِ ﴿٩﴾ |
| 10.Na yatakapodhihirishwa yaliyomo vifuani. | وَحُصِّلَ مَا فِى الصُّدُوْرِ ﴿١٠﴾ |
| 11.Kuwa Mola wao atawajua sana siku hiyo (viumbe vyake). | اِنَّ رَبَّهُمْ بِهِمْ يَوْمَئِذٍ لَّخَبِيْرٌ ﴿١١﴾ |

**Ujumbe wa Suraul-'Adiyat**

Katika sura hii Allah (s.w) anatuhakikishia kuwa mwanaadamu mwenye akili timamu halazimishwi na yeyote kumuasi Allah (s.w). Bali ni yeye mwenyewe anayeamua kuvunja amri za Mola wake kwa ajili ya kufuata matashi ya nafsi yake huku akiwa anafahamu.

Pia sura hii inabainisha jambo jingine la kweli kuwa mwanaadamu anapenda sana mali. Anapenda sana mali kwa sababu humwezesha kujipatia starehe mbali mbali. Starehe ambazo humpelekea mwanaadamu kumuasi Allah (s.w) na kusahau kuwa atakutana naye katika siku ya Hukumu amdhihirishie yale yote aliyoyafanya. Kisha amlipe jaza inayostahiki.

Hivyo kutokana na sura hii tunajifunza kuwa:

(i) Mwanaadamu mwenye akili ni yule anayemwamini Allah (s.w) na kumtii ipasavyo kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake.

(ii) Kila mwanaadamu mwenye akili timamu amepewa uwezo wa Allah (s.w) wa kutambua mazuri na maovu. Hivyo akifanya maovu na kukanusha mazuri atakuwa ana khiyari mwenye kufanya hivyo kwa jeuri. Na hivyo atastahiki adhabu kali katika hiyo siku ya malipo.

(iii) Mali inapotafutwa kwa pupa bila kuzingatia mipaka ya Allah, na inapotumiwa pasina kufuata maelekezo ya Allah au kufanyiwa ubakhili kwa kutowasaidia wenye shida, humsababisha mtu huyo kuwa mkazi wa motoni.

(iv) Pamoja na kupenda sana mali, mtu anapofariki huiacha na hurithiwa na walio hai.

(v) Kila mtu atafufuliwa na kulipwa malipo yaliyo stahiki ya vile alivyotenda na namna alivyochuma na kutumia mali yake.

(vi) Allah anazo khabari sahihi za matendo ya kila mtu, hivyo kila mtu atalipwa kwa uadilifu pasina kudhulumiwa hata chembe.

ina aya 8 | **Suuratul Zilzalah 99** | Makka

| | |
|---|---|
| *Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu.* | بسم الله الرحمن الرحيم |
| 1. Na itakapotetemeshwa ardhi mtetemesho wake (huo mkubwa). | إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ﴿١﴾ |
| 2. Na itakapotoa ardhi mizigo yake. | وَأَخْرَجَتِ الْأَرْضُ أَثْقَالَهَا ﴿٢﴾ |
| 3. Na binaadamu akasema (wakati huo) "(Oh!) ina nini (leo ardhi)?" | وَقَالَ الْإِنْسَانُ مَا لَهَا ﴿٣﴾ |
| 4. Siku hiyo itatoa habari zake (zote). | يَوْمَئِذٍ تُحَدِّثُ أَخْبَارَهَا ﴿٤﴾ |
| 5. Kwa kuwa Mola wake ameifunulia (ameiamrisha kufanya hivyo). | بِأَنَّ رَبَّكَ أَوْحَىٰ لَهَا ﴿٥﴾ |
| 6. Siku hiyo watu watatoka (makaburini) vikundi-vikundi ili waonyeshwe vitendo vyao. | يَوْمَئِذٍ يَصْدُرُ النَّاسُ أَشْتَاتًا لِيُرَوْا أَعْمَالَهُمْ ﴿٦﴾ |
| 7. Basi anayefanya wema (hata) wa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jaza yake. | فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧﴾ |
| 8. Na anayefanya uovu (hata) wa kiasi cha uzito wa mdudu chungu ataona jaza yake. | وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٨﴾ |

**Ujumbe wa Suratul-Zilzal**

Sura hii inatufahamisha baadhi ya matukio ya siku ya kiyama. Ni pamoja na ardhi kutetemeshwa kwa mtetemeko mkubwa, kisha kuwatoa watu wote waliomo ndani yake. Hivyo itakuwa ni siku ya kufufuliwa watu baada ya kufa na kuzikwa humo ardhini kwa kipindi kirefu.

Baada ya kufufuka watu watajikuta katika mazingira magumu. Hapatakuwa na mfalme yeyote ila Allah (s.w) aliye mmoja tu. Mwenye Nguvu na Uwezo atakuwa ni Allah (s.w) peke yake na watu wote watakua ni dhalili na dhaifu mbele yake. Katika Qur-an tunafahamishwa kuwa Allah (s.w) atauliza:

لِّمَنِ ٱلْمُلْكُ ٱلْيَوْمَ ۖ لِلَّهِ ٱلْوَٰحِدِ ٱلْقَهَّارِ ﴿١٦﴾

*… Leo ufalme ni wa nani? (Patakuwa kimya. Kisha Allah (s.w) mwenyewe atajibu) "Ni wa Allah aliye mmoja, Mwenye nguvu". (40:16)*

Kisha watu watakusanywa kwenye uwanja wa hesabu na kila mmoja kulipwa kwa uadilifu. Aliyefanya wema atalipwa kiasi cha wema wake na aliyefanya uovu atalipwa kiasi cha uovu wake.

Katika sura hii tunajifunza:

(i) Tujitahidi kufanya wema kwa kadiri ya uwezo wetu. Wala tusipuuze jema lolote hata likiwa dogo kiasi gani, kwani litalipwa malipo makubwa tutakayoyashangaa.

(ii) Tujitahidi kujiepusha na maovu. Wala tusidharau jambo lolote ovu hata likiwa dogo kiasi gani, kwani hilo linaweza kuwa ndio sababu ya kumuangamiza mtu.

(iii) Hakuna jambo linalofichikana kwa Allah (s.w) kwani mwanaadamu matendo yake yanashuhudiwa na kila kinachomzunguka katika ardhi hii. Na ushahidi huo utatolewa dhidi yetu mbele ya mahakama ya Allah (s.w).

## ZOEZI LA KWANZA

1. (a) Hifadhi kifuani suratul Fat-ha na tafsiri yake.

   (b) Allah ulifahamu kila jambo linaloazimiwa na ________

2. Toa mafunzo yanayopatikana katika suratul Kaafiruuna.

3. Kwa mujibu wa suratun Naas, Jinni au mtu anashawishi watu kufanya maovu huitwa__________

4. Taja mafunzo mawili yanayopatikana katika suratul Aadiyaat.

5.Taja mafunzo matano (5) tunayoyaoata katika suratul Fyl

6. Katika suratul Humazah, watu wenye tabia ya kusengenya na kulimbikiza mali kisha wasiyatolee zakkat na sadaka wataingizwa kwenye moto mkali sana uitwao________

# Somo la 2. Tawhid

## IMANI YA KIISLAMU

### SIFA ZA ALLAH (S.W)

Katika kitabu cha kwanza hadi cha tatu tumethibitisha kuwepo kwa Mungu Muumba ambaye ni Allah (s.w). Tumethibitisha kuwepo kwake kutokana na dalili mbali mbali zinazotokana na maumbile ya mbinguni na ardhini. Pia tumethibitisha kuwa mwanaadamu mwenyewe ni dalili tosha ya kuwepo kwa Allah (s.w).

Haitoshi kuamini tu kuwa yupo Mungu Muumba, bali ni muhimu pia kujua sifa zake zote. Sifa za Allah (s.w) tunazopaswa kuzijua zimebainishwa katika Qur-an na Hadith za Mtume (s.a.w). Katika hadith iliyosimuliwa na Abu Hurairah (r.a) na Ibn Umar (r.a), Mtume (s.a.w) amesema:

*"Kuna majina 99 ya Allah (s.w) atakayeyahifadhi na kuyachambua majina haya, kisha akamuamini Allah (s.w) kwa majina hayo katika kuendesha maisha yake ya kila siku ataingia peponi".* (Muslim) Majina hayo ni:

## 1. Allah: اللّٰهُ

Mwenyezi Mungu, Mola Mwenye kustahiki kuwepo. Hili ndilo jina la Dhati la Mungu Mmoja tu.

## 2. Ar-Rahmaan: الرَّحْمٰنُ

Mwingi wa Rehema (huruma).

## 3. Ar-Rahiim: الرَّحِيْمُ

Mwenye kurehemu.

## 4. Al-Maliku:

الْمَلِكُ

Mfalme wa kweli wa milele. Mfalme wa Wafalme.

## 5. Al-Quddus:

الْقُدُّسُ

Mtakatifu, Ametakasika na sifa zote chafu.

## 6. As-Salaam:

السَّلَامُ

Mwenye Kusalimika, Mwenye kuleta amani, Mwenye Salama.

## 7. Al-Mu'umin:

الْمُؤْمِنُ

Mtoaji wa amani.

## 8. Al-Muhaymin:

الْمُهَيْمِنُ

Mwangalizi wa mambo ya viumbe vyake (matendo yao, uhai wao, n.k) Mlinzi, Mchungaji.

## 9. Al-Aziz:

الْعَزِيزُ

Mwenye Shani, shahidi katika mambo yake, Muhitajiwa wa kila kitu na wala ahitaji kwa yeyote katika viumbe vyake.

## 10. Al-Jabbar:

الجَبَّارُ

Mwenye kuunga mambo yaliyovunjika. Mwenye kulazimisha viumbe wafanye analolitaka yeye bila ya wao kuwa na uwezo wala uhuru wa kumlazimisha yeye kufanya wanalotaka.

## 11. Al-Mutakabbir:

المُتَكَبِّرُ

Mwenye Kibri na Haki ya Kibri

## 12. Al-Khaaliq:

الخَالقُ

Muumbaji, Mbora wa waumbaji, muumbaji wa waumbaji.

## 13. Al-Baariu:

البَارِئُ

Mtengenezaji. Atengenezaye kutoka kwenye hakuna.

## 14. Al-Muswawwir:

المُصَوِّرُ

Mfanyaji wa sura za namna namna

## 15. Al-Ghaffar:

الغَفَّارُ

Msamehevu. Mwenye kusamehe.

## 16. Al-Qahhaaru:

الْقَهَّارُ

Mwenye Nguvu juuya kila kitu asiyepingika.

## 17. Al-Wahhab:

الْوَهَّابُ

Mpaji Mkuu.

## 18. Ar-Razzaaq:

الرَّزَّاقُ

Mtoaji wa Riziki, Mwenye kuruzuku kila kiumbe.

## 19. Al-Fattaah:

الْفَتَّاحُ

Afunguaye kila kitu/jambo. Mfunguzi.

## 20. Al-Aliimu:

الْعَلِيْمُ

Ajuae, Mjuzi wa kila kitu.

## 21. Al-Qaabidh:

الْقَابِضُ

Mwenye kuzuia, Mwenye kufisha na kusababisha kufa, Mwenye kunyima.

## 22. Al-Baasit:

الْبَاسِطُ

Mwenye kutoa, Mwenye kuhuisha, mwenye kuvipa viumbe uhai, mwenye kutajirisha.

**23. Al-Khaafidh:** الخَافِضُ

Mfedhehesha waovu.

**24. Ar-Raafiu:** الرَّافِعُ

Mpaji cheo, Mpandishaji daraja. Mwenye kuimarisha.

**25. Al-Mui'zzu:** المُعِزُّ

Mtoaji heshima kwa amtakaye.

**26. Al-Mudhillu:** المُذِلُّ

Mnyima heshima kwa amtakaye, mwenye kudhili.

**27. As-Samiiu:** السَّمِيعُ

Mwenye kusikia, Msikivu wa hali ya juu kabisa.

**28. Al-Baswiir:** البَصِيرُ

Mwenye kuona, Muoni wa hali ya juu kabisa.

**29. Al-Hakam:** الحَكَمُ

Mwenye kuhukumu, Mwenye kukata shauri, Mwamuzi.

### 30. Al-A'dlu: العَدلُ

Muadilifu, mwenye kutoa haki, asiye dhulumu.

### 31. Al-Latwiif: اللَّطِيفُ

Mpole, laini, mwenye huruma sana.

### 32. Al-Khabiir: الخَبِيرُ

Mwenye khabari zote (mjuzi wa mambo yote).

### 33. Al-haliim: الحَلِيمُ

Mpole sana.

### 34. Al-A'dhiim: العَظِيمُ

Mkuu, Mtukufu.

### 35. Al-Ghafuur: الغَفُورُ

Msamehevu.

### 36. Ash-Shakuur: الشَّكُورُ

Mwenye shukrani.

## 37. Al-A'Iliyyu:

العَلِيُّ

Aliye juu .

## 38. Al-Kabiir:

الكَبِيْرُ

Mkubwa wa kuishi, Mkongwe.

## 39. Al-Hafiidh:

الحَفِيْظُ

Mwenye kuhifadhi kila kitu. Mtunzaji.

## 40. Al-Muqiitu

المُقِيْتُ

Mlishaji, Mtoaji Riziki kwa kila kiumbe, Mwenye nguvu.

## 41. Al-Hasiib:

الحَسِيْبُ

Mwenye kuhesabu, Mjuzi wa Hesabu.

## 42. Al-Jaliil:

الجَلِيْلُ

Mzuri wa hali ya juu, Tajiri, Mtukufu, Mjuzi, Mtawala, mwenye Nguvu.

## 43. Al-Kariim:

الكَرِيمُ

Mtukufu mwenye ukarimu.

## 44. Ar-Raqiibu: الرَّقِيْبُ

Mwenye kuona yote yanayofikiriwa, yanayofanywa, na yanayotukia.

## 45. Al-Mujiibu: الْمُجِيْبُ

Mpokeaji wa maombi ya waja wake. Hupokea nia, jitihada za waja na matendo yao.

## 46. Al-Waasiu: الوَاسِعُ

Mwenye Wasaa, Mwenye kila kitu. Humiliki vilivyopo na visivyokuwepo.

## 47. Al-Hakiim: الحَكِيمُ

Mwenye Hikma. Chanzo cha hekima.

## 48. Al-Waduud: الوَدُوْدُ

Mwenye Upendo Mwenye kupenda kuwatakia mazuri watu.

## 49. Al-Majiidu: المَجِيْدُ

Mtukufu  Mwenye kustahiki kutukuzwa.

## 50. Al-Baa'ithu: الْبَاعِثُ

Mwenye kufufua wafu.

## 51. As-Shahiidu: الشَّاهِدُ

Shahidi mwenye kushuhudia kila kitu

## 52. Al-Haqqu: الْحَقُّ

Wa haki, Wa kweli hasa, Mkweli

## 53. Al-Wakiilu: الوَكِيْلُ

Wakili , Mdhamini,Mlinzi mwenye kustahiki kuachiwa mambo ya watu. Mtetezi.

## 54. Al-Qawiyyu: القَوِيُّ

Mwenye nguvu. Chanzo cha nguvu zote.

## 55. Al-Matiinu: المَتِينُ

Aliye Madhubuti Asiyetingishika kwa lolote. Haathiriki.

## 56. Al-Waliyyu: الوَلِيُّ

Mwenye kusifika, kila sifa njema ni zake.

## 57. Al-Hamiidu:

الْحَمِيْدُ

Rafiki Mlinzi, Mlinzi na Msaidizi, Mlezi

## 58. Al-Muhswy:

الْمُحْصِي

Mwenye kudhibiti (hesabu), Mwenye kuhesabu.

## 59. Al-Mubdiu:

الْمُبْدِئُ

Mwenye kuanzisha.

## 60. Al-Mu'iid:

الْمُعِيْدُ

Mwenye kurejeza. Yeye Allah Ndiye Mwenye kuanzisha viumbe na kuvifanya vifu, kisha ndiye mwenye kuvirejesha tena kwenye maisha baada ya kufa.

## 61. Al-Muhyi:

الْمُحْيِي

Mwenye kuhuisha.

## 62. Al-Mumiitu:

الْمُمِيْتُ

Mwenye kufisha

## 63. Al-Hayyu:

الحَيُّ

Mwenye uhai wa milele

## 64. Al-Qayyum:

القَيُّوْمُ

Msimamia kila jambo, Mwendeshaji wa mambo yote.

## 65. Al-Waajidu:

الوَاجِدُ

Mwenye utambuzi wa kila kitu. Mtambuzi

## 66. Al-Maajidu:

المَاجِدُ

Wa kuheshimiwa, Mtukufu

## 67. Al-Waahidu:

الوَاحِدُ

Mwenye kupwekeka, Mmoja tu

## 68. As-Swamadu:

الصَّمَدُ

Mwenye kukusudiwa kwa kuabudiwa, kuombwa na kutegemewa.

## 69. Al-Qaadiru:

القَادِرُ

Mwenye uwezo wa kufanya au kutofanya kila kitu, Muweza wa kufanya au kutofanya chochote.

## 70. Al-Muqtadiru: الْمُقْتَدِرُ

Mwenye kudiriki kila kitu, mwenye uwezo wa pekee juu ya kila kitu

## 71. Al-Muqaddimu: الْمُقَدِّمُ

Mwenye kutanguliza, mwenye kumleta mja karibu naye.

## 72. Al-Muakhiru: الْمُؤَخِّرُ

Mwenye kuakhirisha. Mwenye kubakisha nyuma, Mwenye kumpeleka mja mbali naye

## 73. Al-Awwalu: الأَوَّلُ

Wa mwanzo.

## 74. Al-Aakhiru: الأَاخِرُ

Wa mwisho.

## 75. Adh-Dhaahiru: الظَّاهِرُ

Wa dhahiri. Hujulikana kupitia alivyoviumba.

## 76. Al-Baatwinu:

Wa siri. Haonekani kwa macho.

الْبَاطِنُ

## 77. Al-Walii:

Gavana , Mpanga Mipango ya watu na mwangalizi wa mipango yote.

الْوَالِي

## 78. Al-Muta'aali:

Mtukufu aliye juu

الْمُتَعَالِي

## 79. Al-Barru:

Mwema

الْبَرُّ

## 80. At-Tawwaabu:

Mwenye kupokea Toba za waja wake.

التَّوَّابُ

## 81. Al-Muntaqimu:

Mwenye kuchukua kisasi, Mlipa kisasi kwa waovu.

الْمُنْتَقِمُ

## 82. Al-A'fuwwu:

Mwenye kusamehe madhambi, mfuta madhambi ya waja wake Msamehevu.

الْعَفُوُّ

## 83. Ar-Rauuf:

الرَّءُوفُ

Mpole, Mwenye huruma

## 84. Maalikul-Mulk:

مَالِكُ الْمُلْكِ

Mwenye kumiliki ufalme wote, Mfalme wa Wafalme Mwenye kutumia mamlaka yake atakavyo.

## 85. Dhul-jalaali Wal-Ikraami:

ذُوْ جَلَالِ وَالإِكْرَامِ

Mwenye Utukufu na Heshima

## 86. Al-Muqsitu:

الْمُقْسِطُ

Mwenye kukamilisha usawa Mwenye kutoa usawa, Mtoaji Haki sawa kwa kila anayestahiki.

## 87. Al-Jaami'u:

الْجَامِعُ

Mkusanyaji Mkusanyaji viumbe siku ya mwisho (Kiyama).

## 88. Al-Ghaniyyu:

الْغَنِيُّ

Mwenye kujitosheleza, Hahitaji chochote kwa yeyote , Tajiri.

## 89. Al-Mughnii: الْمُغْنِي

Mwenye kutajirisha, mwenye kutosheleza viumbe kwa kila wanachohitajia.

## 90. Al-Maani'u: الْمَانِعُ

Mwenye kusalimisha viumbe kutokana na mabaya, mwenye kuzuia viumbe visidhurike, mwenye kunusuru

## 91. Adh-Dhaar: الضَّارُّ

Mwenye kuleta shari (Dhara), Mwenye kudhurisha

## 92. An-Naafi'u: النَّافِعُ

Mwenye kuleta nafuu (Kheri), Mwenye kunufaisha

## 93. An-Nuur: النُّوْرُ

Nuru, Mwenye Nuru, Mwangaza .

## 94. Al-Haadi: الهَادِى

Mwenye kuongoza waja wake katika kheri mbali mbali, Mwongozaji

### 95. Al-Badii'u: البَدِيْعُ

Mwasisi. Mwanzilishi.

### 96. Al-Baaqiy: البَاقِيْ

Mwenyekubakia Milele, hana mwisho .

### 97. Al-Waarithu: الوَارِثُ

Mrithi, Mwenye Kurithi kila kitu

### 98. Ar-Rashiidu: الرَّشِيْدُ

Mwenye kuongoa, mwenye kuongoa waja wake kuiendea njia ya kheri.

### 99. As-Swabuuru: الصَّبُوْرُ

Mwenye kusubiri, mwenye subira

Utaona kuwa katika haya majina 99, jina la dhati la Mwenyezi Mungu ni moja nalo ni Allah. Majina yote 98 yaliyobakia ni sifa zake.

**Matumizi ya majina ya Allah (s.w)**

Tunatakiwa tuyatumie majina ya Allah (s.w) katika kumuomba na kujitegemeza kwake. Tusiombe dua zetu kwa jina la kiumbe chochote. Wala tusiombe dua zetu kwa baraka za asiyekuwa Allah(s.w). Bali tuombe kwa majina matukufu ya Allah (s.w) kama anavyotuamrisha katika Qur-an:

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا

*Na Allah ana majina mazuri mazuri, muombeni kwayo… (7:180)*

قُلِ ادْعُوا اللَّهَ أَوِ ادْعُوا الرَّحْمَٰنَ ۖ أَيًّا مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ
الْحُسْنَىٰ ۚ وَلَا تَجْهَرْ بِصَلَاتِكَ وَلَا تُخَافِتْ بِهَا وَابْتَغِ بَيْنَ
ذَٰلِكَ سَبِيلًا ﴿١١٠﴾

*Sema: Muombeni (Mwenyezi Mungu) kwa (jina la) Allah au muombeni (kwa jina la) Rahman, kwa jina lolote mnalomwita (katika haya litafaa) kwani ana majina mazuri mazuri… (17:110)*

Kwa mfano ukitaka kumuomba Allah akuzidishie rizki uanze kumuomba: "*Yaa Razzaaq…*", ukitaka akuzidishie elimu anza kuomba: "*Yaa Aliim…*", ukitaka akuondolee khofu au wasiwasi anza kuomba, "*Yaa Ssalaam…*", ukitaka akusamehe makosa yako anza kuomba: "*Yaa Ghaffaaru…*".

Tunaomba kwa majina ya Allah (s.w) kwa sababu ndiye mwenye uwezo juu ya kila kitu. Yeye pekee ndiye mwenye uwezo wa kututosheleza kwa kila tunalolihitajia. Tumeamrishwa tumtegemee Allah peke yake.

**Sifa za Allah (s.w) katika Qur-an:**

Aya za Qur-an zinazobainisha baadhi ya majina ya Allah (s.w) kwa mfululizo ni hizi zifuatazo:

**1. Ayatul-Qursiyyu**

ٱللَّهُ لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ٱلْحَىُّ ٱلْقَيُّومُ ۚ لَا تَأْخُذُهُۥ سِنَةٌ وَلَا نَوْمٌ ۚ
لَّهُۥ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ ۗ مَن ذَا ٱلَّذِى يَشْفَعُ عِندَهُۥٓ
إِلَّا بِإِذْنِهِۦ ۚ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ ۖ وَلَا يُحِيطُونَ
بِشَىْءٍ مِّنْ عِلْمِهِۦٓ إِلَّا بِمَا شَآءَ ۚ وَسِعَ كُرْسِيُّهُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ
وَٱلْأَرْضَ ۖ وَلَا يَـُٔودُهُۥ حِفْظُهُمَا ۚ وَهُوَ ٱلْعَلِىُّ ٱلْعَظِيمُ ﴿٢٥٥﴾

*Allah hakuna Mola ile Yeye, Mwenye Uhai wa Milele, msimamia kila jambo. Kusinzia kwake hakumshiki wala kulala. Ni vyake peke yake vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na nani huyo awezaye kushufaia (kuombea) mbele yake bila ya idhini yake? Anayajua yaliyo mbele yao (viumbe) na yaliyo) nyuma yao; wala hao viumbe hawajui lolote katika ilimu yake ila kwa alipendalo lijulikane. Enzi yake imeenea mbinguni na ardhini wala kuvilinda hivyo hakumshindi. Ni Yeye pekee ndiye aliye juu, aliye Mkuu. (2:255)*

Maneno yaliyokolea wino ni katika majina ya Allah (s.w). Kwa muhtasari aya hii inatufahamisha yafuatayo:

(i) Mungu ni Mmoja tu naye ni Allah (s.w).

(ii) Allah (s.w) Yu Hai Milele. Yaani si mwenye kufa au kutoweka. Bali ni mwenye kubakia milele (muda wote).

(iii)Allah (s.w) hasinzii wala halali. Yaani kila wakati Allah (s.w) yuko macho au yuko hadhiri.

(iv)Allah (s.w) ndiye anayemiliki vitu vyote vilivyomo mbinguni na ardhini.

(v) Allah (s.w) ni Mjuzi wa kila kitu. Anajua yote yaliyopita na yote yajayo. Hapana jambo asilolijua.

(vi)Allah (s.w) ni Mfalme wa kila kitu. Hapana awezaye kuweka ulinzi pale alipoutoa Allah (s.w) na wala hapana awezae kuharibu ulinzi aliouweka Allah (s.w)

(vii) Allah (s.w) Ndiye Pekee aliye juu kwa utukufu kuliko yeyote yule.

(viii)Allah (s.w) ni Mkuu juu ya kila kitu, mwenye kutawala vitu vyote.

## 2. Suratul-Hadyd

سَبَّحَ لِلَّهِ مَا فِي ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۖ وَهُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ ﴿١﴾ لَهُۥ مُلْكُ
ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۖ يُحْيِۦ وَيُمِيتُ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٢﴾
هُوَ ٱلْأَوَّلُ وَٱلْءَاخِرُ وَٱلظَّٰهِرُ وَٱلْبَاطِنُ ۖ وَهُوَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ ﴿٣﴾

*Kinamtukuza Allah kila kilichomo mbinguni na ardhini, na Yeye ndiye Mwenye nguvu, Mwenye Hikima, Ufalme wa mbinguni na ardhini ni wake. Anahuisha na kufisha. Naye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.Yeye ndiye wa Mwanzo na ndiye wa Mwisho, naye ndiye wa Dhahiri na wa siri, naye Mjuzi wa kila kitu.*

هُوَ ٱلَّذِي خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ ٱسْتَوَىٰ
عَلَى ٱلْعَرْشِ ۚ يَعْلَمُ مَا يَلِجُ فِي ٱلْأَرْضِ وَمَا يَخْرُجُ مِنْهَا وَمَا يَنزِلُ مِنَ
ٱلسَّمَآءِ وَمَا يَعْرُجُ فِيهَا ۖ وَهُوَ مَعَكُمْ أَيْنَ مَا كُنتُمْ ۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ
بَصِيرٌ ﴿٤﴾

لَهُۥ مُلْكُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۚ وَإِلَى ٱللَّهِ تُرْجَعُ ٱلْأُمُورُ
﴿٥﴾ يُولِجُ ٱلَّيْلَ فِى ٱلنَّهَارِ وَيُولِجُ ٱلنَّهَارَ فِى ٱلَّيْلِ ۚ
وَهُوَ عَلِيمٌۢ بِذَاتِ ٱلصُّدُورِ ﴿٦﴾

*Yeye ndiye aliyeziumba mbingu na ardhi katika nyakati sita, kisha akakaa katika enzi yake. Anayajua yanayoingia katika ardhi na yanayotoka humo. Naye yu pamoja nanyi popote mlipo. Na Allah anayaona mnayoyatenda yote. Ufalme wa mbingu na ardhi ni wake. Na mambo yote yanarudishwa kwa Allah. Anaingiza usiku katika mchana na anaingiza mchana katika usiku. Na yeye anajua yaliyomo vifuani. (57:1-6)*

Kwa muhtasari aya hizi zinatufahamisha sifa za Allah (s.w) kama ifuatayo:

(a) Allah (s.w) ndiye pekee anayestahiki kutukuzwa na kila kilicho mbinguni na ardhini.

(b) Allah (s.w) ni Mwenye kumiliki nguvu za viumbe. Nguvu zote hutoka kwake.

(c) Allah (s.w) ni Mwenye Hikima kubwa isiyo na kikomo.

(d) Allah (s.w) amekuwepo nyakati zote. Yaani hapana wakati ambao hakuwepo. Ndiye mwanzo na mwisho.

(e) Allah (s.w) ni mwenye kudumu. Yaani Yeye ni Mwenye kubakia milele. Allah (s.w) ni wa tangu na tangu na atabakia kuwepo milele na milele.

(f) Ufalme wa mbinguni na ardhini uko mikononi mwa Allah (s.w). wafalme wote wa ulimwenguni ni wa bandia. Mfalme wa kweli ni Allah (s.w).

(g) Allah (s.w) ndiye pekee anayefisha. Hapana mwenye uwezo wa kumfisha mtu kinyume na idhini ya Allah (s.w). Hivyo mtu asiogope kifo bali amuogope Allah (s.w).

(h) Allah (s.w) haonekani wazi wazi kwa macho yetu, bali sifa zake na utukufu wake hudhihirika katika maumbile ya maisha ya ulimwengu.

(i) Allah (s.w) ni mjuzi wa kila kilicho mbinguni na ardhini. Hakuna hata kimoja kidogo au kikubwa kinachofichikana kwake. Hakuna habari ndogo au kubwa asiyoijua. Hakuna siri mbele ya Allah (s.w). Analiona na analijua tunalolifanya kwa siri au kwa dhahiri. Allah(s.w) hisia, fikira na dhamira za kila mtu.

(j) Allah (s.w) ndiye anayeleta usiku na mchana.

(k) Allah (s.w) ni mjuzi wa siri zilizofichikana vifuani mwetu.

(l) Allah (s.w) ndiye marejeo ya wanaadamu wote na viumbe vyote.

## 3. Suratul-Hashr

هُوَ ٱللَّهُ ٱلَّذِى لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ عَٰلِمُ ٱلْغَيْبِ وَٱلشَّهَٰدَةِ ۖ
هُوَ ٱلرَّحْمَٰنُ ٱلرَّحِيمُ ﴿٢٢﴾ هُوَ ٱللَّهُ ٱلَّذِى لَآ إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ
ٱلْمَلِكُ ٱلْقُدُّوسُ ٱلسَّلَٰمُ ٱلْمُؤْمِنُ ٱلْمُهَيْمِنُ ٱلْعَزِيزُ
ٱلْجَبَّارُ ٱلْمُتَكَبِّرُ ۚ سُبْحَٰنَ ٱللَّهِ عَمَّا يُشْرِكُونَ
﴿٢٣﴾ هُوَ ٱللَّهُ ٱلْخَٰلِقُ ٱلْبَارِئُ ٱلْمُصَوِّرُ ۖ لَهُ ٱلْأَسْمَآءُ ٱلْحُسْنَىٰ ۚ
يُسَبِّحُ لَهُۥ مَا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ ۖ وَهُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْحَكِيمُ ﴿٢٤﴾

*Yeye ni Allah ambaye hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye tu. Anayajua yaliyofichikana na yaliyo dhahiri, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Kurehemu. Yeye ni Allah ambaye hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu,*

*Mwenye Salama, Mtoaji wa Amani, Mwenye kuyaendesha mwenyewe mambo yake, Mwenye Shani, Mwenye Kibri (afanyaye analolitaka) Allah yu mbali na hao wanaomshirikisha naye. Yeye ni Allah, Muumbaji, Mtengenezaji, Msanifu (mtengenezaji wa sura mbali mbali) Mwenye sifa nzuri nzuri. Kinamtukuza kila kilichomo mbinguni na ardhini. Naye ni Mwenye nguvu, Mwenye Hikima. (59:22-24)*

4. **Suratul-Ikhlas**

قُلْ هُوَ ٱللَّهُ أَحَدٌ ﴿١﴾ ٱللَّهُ ٱلصَّمَدُ ﴿٢﴾
لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ ﴿٣﴾ وَلَمْ يَكُن لَّهُۥ
كُفُوًا أَحَدٌۢ ﴿٤﴾

*Sema: Yeye ni Allah aliye mmoja tu. Allah (tu pekee) ndiye anayestahiki kukusudiwa (kwa kuabudiwa, kuombwa na kutegemewa). Hakuzaa wala hakuzaliwa. Wala hana anayefanana naye hata mmoja. (112:1-4)*

Sura hii imeitwa sura ya utakaso. Inabainisha kuwa Allah (s.w) ametakasika na sifa pungufu. Tunajifunza kutokana na sura hii kuwa

(a) Allah ni jina la dhati la Mwenyezi Mungu pekee (s.w).

(b) Allah (s.w) ndiye anayestahiki kuabudiwa, kuombwa na kutegemewa.

(c) Allah (s.w) hana mtoto. Yu mbali kabisa na sifa hiyo duni ya kuwa na mtoto.

(d) Allah (s.w) si mzaliwa wa yeyote. Yeye mwenyewe ni mwanzo na chanzo cha kila kitu.

(e) Allah (s.w) hana mfano wa chochote. Tusijisumbue kumfikiri Allah (s.w) kwa kumfananisha na chochote. Kwani hafanani na chochote tunachoweza kufikiria.

**Maana ya Kumuamini Allah (s.w) katika maisha ya kila siku**

Imani ya kweli juu ya Allah (s.w) haina budi kudhihirishwa katika matendo ya maisha ya kila siku. Muumini wa kweli ni yule mwenye yakini moyoni juu ya kuwepo Allah (s.w) na sifa zake tukufu.

Kisha huishi katika maisha yake yote kwa kutekeleza maamrisho yote ya Allah (s.w) na kuacha makatazo yake yote. Maamrisho ya Allah (s.w) ni kama vile kusimamisha swala, kufunga ramadhani, kutoa Zakat na Sadakat, kuwafanyia wema wazazi, kuwahurumia na kuwafanyia watu wema, nakadhalika. Matakatazo ya Allah (s.w) ni kama vile kulewa, kusema uongo, kusengenya watu na maovu mengine mbali mbali.

**Kumshirikisha Allah (s.w)**

Kumshirikisha Allah (s.w) ni kumjaalia Allah (s.w) kuwa na wasaidizi au washirika katika Uungu wake. Kitendo cha kumjaalia Allah (s.w) kuwa na wasaidizi au washirika ni kitendo cha kumdunisha Allah (s.w).

Kumjaalia Allah (s.w) kuwa hana uwezo wa kuvimiliki, kuviongoza na kuvitosheleleza viumbe vyake alivyoviumba mwenyewe. Kumshirikisha Allah (s.w) ni kosa kubwa sana mbele ya Allah (s.w) kama tunavyojifunza katika Qur-an:

إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِۦ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ
لِمَن يَشَآءُ ۚ وَمَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱفْتَرَىٰٓ إِثْمًا
عَظِيمًا ﴿٤٨﴾

*Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishwa na husamehe yasiyokuwa haya kwa amtakaye. Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu bila shaka amebuni dhambi kubwa. (4:48)*

Katika jamii, watu huweza kumshirikisha Allah (s.w) kwa namna kuu nne. Aina hizi za shirki ni:

(i) Shirki katika DHATI ya Allah (s.w)

(ii) Shirki katika SIFA za Allah (s.w)

(iii) Shirki katika MAMLAKA za Allah (s.w)

(iv) Shirki katika HUKUMU za Allah (s.w)

**(i) Shirki ya Dhati**

Kumshirikisha Allah (s.w) katika dhati yake ni kukijaalia kiumbe kuwa ni mungu kama vile sanamu, jua, hirizi, jiwe na kukiomba na kukitegemea.

**(ii) Shirki ya Sifa**

Kumshirikisha Allah (s.w) katika Sifa zake ni kukisifu kiumbe chochote kwa sifa za Allah (s.w) kama vile kumjaalia mtu kuwa anajua mambo ya ghaibu, anatoa riziki, anaweza kuwa kila mahali n.k.

Pia kumjaalia Allah (s.w) kuwa na sifa za viumbe kama vile kuzaa au kuzaliwa ni katika shirki ya Sifa.

**(iii) Shirki ya Mamlaka**

Kumshirikisha Allah (s.w) katika Mamlaka ni kumtii kiumbe kinyume na maamrisho au makatazo ya Allah (s.w) kama vile kukatazwa kuswali na mwalimu na wewe ukamtii. Utakapo mtii mwalimu kinyume na Allah (s.w) utakuwa umemfanya mwalimu kuwa mungu wako. Ndivyo tunavyofahamishwa katika Qur-an:

اتَّخَذُوٓا۟ أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَٰنَهُمْ أَرْبَابًا
مِّن دُونِ ٱللَّهِ

*(Mayahudi na Wakristo) wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni miungu badala ya Mwenyezi Mungu… (9:31)*

Katika kufafanua aya hii Mtume (s.a.w) amesema kuwa wameshutumiwa hivyo kwa sababu watu waliwatii viongozi wao kinyume na maamrisho ya Allah (s.w).

**(iv) Shirki ya Hukumu**

Kumshirikisha Allah (s.w) katika Hukumu zake, ni kuwahukumu watu waliofanya makosa kinyume na hukumu aliyoitoa Allah (s.w) kwa makosa hayo. Kwa mfano, watu wakiamua kumpiga mwizi, kumchoma moto, kumwua au kumfunga jela, watakuwa wanamshirikisha Allah (s.w).



## Zoezi la Pili

1. Orodhesha majina ya Allah (s.w) yanayoonesha kuwa yeye ndiye Muumba.

2. Taja majina ya Allah (s.w) yanayoonesha kuwa yeye hafichwi jambo

3. Bainisha majina ya Allah (s.a.w) yanayoonesha kuwa analotaka yeye ndilo huwa

4. Taja sifa za Allah (s.w) zinazokanusha kuwa Yeye si nabii Isa/Yesu.

5. Kumshirikisha Allah (s.w) maana yake nini?

6. Taja matendo ambayo mtu akiyafanya atakuwa anamshirikisha Allah (s.w)

7. Nukuu aya inayobainisha kuwa kumshirikisha Allah (s.w) kwa makusudi ni dhambi kubwa sana.

8. Eleza maana ya istilahi zifuatazo:

    (a) Shirki ya dhati

    (b) Shirki ya sifa

    (c) Shirki ya mamlaka

    (d) Shirki ya hukumu.

# KUSIMAMISHA SWALA

## TWAHARA

Twahara ni utakaso wa mwili na nafsi. Nguo yenye najsi si twahara. Mswala wenye najsi si twahara. Ukiingiwa na najsi mwilini huna twahara. Wakati wa kwenda haja ndogo tuwe waangalifu tusirukiwe na najsi. Tukienda haja tuchuchumae na kustanji viziri ili tusijipakaze najsi tukakosa kuwa twahara.

Tunatwaharisha nguo zetu na miili yetu kutokana na najsi kwa kutumia maji safi. Tunatwaharisha nafsi zetu kwa kutia udhu huku tukiwa tunamzingatia Allah (s.w). Mtume (s.a.w) amesema:

> *Hana udhu yule ambaye hamzingatii Allah (s.w) wakati wa kutawadha.*

Tukitawadha tusizungumze ili tuweze kumzingatia Allah (s.w). Mtu asiye na udhu hawezi kuswali kwa sababu si twahara. Mtu aliye na najsi hawezi kuswali kwa sababu si twahara. Hapana swala bila twahara. Mtume (s.a.w) amesema:

> *"Ufunguo wa Pepo ni Swala na Ufunguo wa Swala ni Twahara".*

### Kutayammamu

Kutayammamu ni kutia udhu kwa kutumia udongo safi badala ya maji safi. Udongo safi pia hutumika katika kuondolea najsi kubwa. Udongo safi ni udongo wenye sifa zifuatazo:

(i) Udongo usio na najsi.

(ii) Udongo usiochanganyika na kitu kingine kisichokuwa asili yake kama vile vumbi la mkaa, sementi, unga na kadhalika.

**Sababu za kuruhusiwa kutayammamu**

Allah (s.w) ameturuhusu kutayammamu iwapo:

(1) Tumekosa maji kabisa.

(2) Tukiwa safarini tukawa tumekosa maji au hatuwezi kutumia maji ndani ya vyombo tunavyosafiria.


(3) Tukiwa na ugonjwa usio ruhusu kutumia maji.

**Namna ya Kutayammamu**

Viungo vya faradhi tunavyoviosha wakati wa kutia udhu ni uso, mikono mpaka vifundoni, kupaka maji kichwani na miguuni mpaka vifundoni.

Kutayammamu tunapaka vumbi la udongo safi uso na mikono mpaka vifundoni. Tunatayammamu kwa kufuata utaratibu ufuatao:

1. Kutayarisha udongo safi wenye vumbi vumbi. Usiwe umelowa. Kisha tia nia ya kutayammamu moyoni.
2. Piga udongo kwa viganja vyote viwili – pigo la kwanza.
3. Kung'uta vizuri viganja kwa pembeni mbali na udongo unaotumia mpaka udongo wote uishe mikononi.
4. Paka uso wote kwa viganja vyote.
5. Piga tena udongo kwa viganja vyote viwili – pigo la pili.
6. Kung'uta vizuri viganja kwa pembeni mbali na udongo unaotumia mpaka udongo wote uishe mikononi.
7. Anza kupaka mkono wa kulia kwa kiganja cha mkono wa kushoto. Anzia kwenye ncha za vidole kwa nyuma mpaka kwenye fundo kisha kwa mbele kwenye kidole gumba. Hakikisha hukigusi kiganja cha mkono wa kulia.
8. Kwa namna hiyo hiyo paka mkono wa kushoto kwa kiganja cha mkono wa kulia.


TAYAMAMU
1
2
3
4
5
6
7

Baada ya kwisha kutayammamu utasoma dua kama ile tuliyoisoma baada ya kutia udhu katika kitabu cha tatu.

**Masharti ya Kutayammamu**

Muislamu anaweza kutia udhu wakati wowote. Ni vizuri hasa kuwa na udhu kila wakati. Lakini udhu wa tayammamu si wenye kudumu kama ule uliopatikana kwa kutumia maji. Hivyo udhu wa tayammamu unakamilika na kubakia kwa kufuata masharti yafuatayo:

1. Pawe na sababu ya kutayammamu (rejea sababu za kutayammamu).

2. Pawe na haja ya kutayammamu kama vile kuswali swala ya faradhi ambayo wakati wake umeshaingia, kuswali swala ya sunnah au kutufu kwenye Ka'aba huko Makka.

3. Pawe na udongo safi ulio mkavu.

**Kutenguka kwa udhu wa tayammamu**

Udhu uliopatikana kwa kutayammamu hubatilika kwa kupatikana mojawapo ya haya yafuatayo:

1. Kufikwa na jambo linalotengua udhu kama tulivyojifunza katika kitabu cha tatu.

2. Kupatikana maji kama ulitayammamu kwa kukosa maji.

**Kusimamisha Swala**

Swala husimama kwa kukamilisha mambo maalum matatu yafuatayo:

1. Kutekeleza sharti zote za swala.

2. Kutekeleza nguzo zote za swala.

3. Kuwa mnynyekevu kwa Allah (s.w) wakati wa kuswali.

**Sharti za Swala**

Muislamu hawezi kuswali mpaka kwanza atekeleze masharti yafuatayo:

(a) Aepukane na najsi kubwa na ndogo katika mwili, nguo na mahali pa kuswalia.

(b) Awe na udhu.

(c) Awe amejisitiri vizuri.

(d) Swala ya faradhi anayoiswali iwe ni katika wakati wake.

(e) Awe amesimama na kuelekea Qibla wakati wa kuswali.

**Nguzo za Swala**

Katika kitabu cha tatu tulijifunza kuwa kuna nguzo 17 za swala. Nguzo hizi zimegawanyika katika mafungu makubwa matatu:

(a) Nguzo ya moyoni (nia).

(b) Nguzo za visomo au matamshi.

(c) Nguzo za vitendo.

**(a) Nguzo ya Moyoni**

Nia ni nguzo inayotekelezwa moyoni. Nia si matamshi bali ni dhamira inayokuwa moyoni kuwa unadhamiria kuswali swala fulani.

**(b) Nguzo za visomo au matamshi**

Nguzo za matamshi ni zile zinazopatikana kwa kutamka. Nguzo hizi ni tano kama ifuatavyo:

(i) Takbira ya kuhirimia au kusema *Allahu akbar* wakati wa kuanza swala.

(ii) Kusoma Suratul-Fat-ha (al-Hamdu).

(iii) Kusoma Tahiyyatu.

(iv) Kumswalia Mtume.

(v) Kutoa salaam mwisho wa swala.

**(c) Nguzo za matendo**

Nguzo 11 zilizobakia ni nguzo za matendo zifuatazo:

(i) Kurukuu.

(ii) Kujituliza katika rukuu.

(iii) Kuitidali.

(iv) Kujituliza katika itidali.

(v) Kusujudu sijida ya kwanza.

(vi) Kujituliza katika sijida ya kwanza.

(vii) Kukaa kati ya sijida mbili.

(viii) Kujituliza katika kikao hicho.

(ix) Kusujudu katika sijida ya pili.

(x) Kujituliza katika sijida ya pili.

(xi) Kukaa tahiyyatu.

**Namna Mtume (s.a.w) alivyoswali**

Mtume Muhammad (s.a.w) amesisitiza kuwa tuswali kama yeye alivyoswali. Kutokana na Hadith mbali mbali tunajifunza kuwa Mtume (s.a.w) aliswali kama ifuatayo:

1. Alitia moyoni nia ya kuswali swala iliyo mbele yake.

2. Alianza swala kwa takbira (Allahu Akbar).

3. Kisha alishusha mikono yake na kuifunga kifuani.

4. Alisoma dua ya kufungulia swala. Rejea dua hii katika kitabu cha tatu.

5. Kabla ya kuanza suratul-Fat-ha, alisoma "*Au'dhubillah Minash shaitwaanir-Rajiim*".

6. Alisoma Suratul-Fat-ha (al-Hamdu).

7. Katika rakaa ya kwanza na ya pili alisoma sura au aya za Qur-an baada ya Suratul-Fat-ha.

8. Alitoa takbira (alisema Allahu Akbar) kila alipokuwa anabadilisha vitendo isipokuwa kwenye kuitidali.

9. Alirukuu na kusema "Sub-haana Rabill-A'dhiim" mara tatu.

10. Aliitidali na kusema wakati anainuka "Samia'llahu limanhamidah" na aliposimama wima aliongezea "Subhana Rabbil-A-A'laa" mara tatu.

11. Alisujudu kwa kugusa paji la uso wake chini

12. Alikaa kikao cha kati ya sijida mbili na kusema "Rabbiighufiriliy Wah-diniy Waafniy".

13. Alisujudu sijida ya pili na kuleta tasbihi kama alivyofanya katika sijida ya kwanza.

14. Baada ya rakaa mbili, alikaa tahiyaatu na kuisoma mpaka mwisho (rejea kitabu cha 2 na 3).

15. Alimswalia Mtume baada ya kusoma tahiyyatu katika rakaa ya mwisho.

16. Alisoma dua kabla ya kutoa salamu (rejea dua hii katika kitabu cha tatu).

17. Alitoa salaam ya kwanza na kugeuza kichwa upande wa kulia, kisha alitoa salaam ya pili na kugeuzia kichwa upande wa kushoto.

**Sijidatu-Sahau (sijda za kusahau)**

Sijida za kusahau ni sijida mbili zinazoletwa mwishoni mwa swala kabla ya kutoa salaam ili kufidia kitendo cha sunna (kisicho cha nguzo) kilichosahauliwa, kwa mfano kusahau kukaa tahiyyatu ya kwanza. Pia sijida za kusahau huletwa ili kusawazisha rakaa iliyozidishwa kwa kusahau.

**Sijidatut-Tilaawat (sijida ya kisomo)**

Sijida ya kisomo ni sijida inayoletwa mara tu baada ya kusoma aya ya Qur-an inayoashiria sijida. Sijida hii huletwa ukiwa ndani ya swala au nje ya swala. Ukiwa ndani ya swala utasujudu mara tu baada ya kusoma aya hiyo inayoashiria sijida. Kisha utasimama na kuendelea na swala yako kama kawaida. Katika aya zinazoashiria sijida ni hizi zifuatazo:

1. Sura ya 7 aya ya 206 (7:206)

2. Sura ya 13 aya ya 15 (13:15)
3. Sura ya 16 aya ya 50 (16:50)
4. Sura ya 17 aya ya 109 (17:109)
5. Sura ya 19 aya ya 58 (19:58)
6. Sura ya 22 aya ya 18 (22:18)
7. Sura ya 22 aya ya 77 (22:77)
8. Sura ya 25 aya ya 60 (25:60)
9. Sura ya 27 aya ya 26 (27:26)
10. Sura ya 32 aya ya 15 (32:15)
11. Sura ya 38 aya ya 24 (38:24)
12. Sura ya 41 aya ya 38 (41:38)
13. Sura ya 53 aya ya 62 (53:62)
14. Sura ya 84 aya ya 21 (84:21)
15. Sura ya 96 aya ya 19 (96:19)

Kila Mtume (s.a.w) aliposoma aya hizi alileta sijda ya kisomo akiwa ndani au nje ya swala maadamu tu anaudhu. Hivyo hatuna budi kumuigiza Mtume kwa kusujudu kila tunaposoma aya hizo.

**Unyenyekevu katika Swala (Khushui)**

Swala hukamilika kwa kupatikana uyenyekevu au khushui wakati wa kuswali. Allah (s.w) anatufahamisha katika Qur-an:

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَاتِهِمْ
خَٰشِعُونَ ﴿٢﴾

*Hakika wamefuzu waumini ambao katika swala zao huwa wanyenyekevu. (23:1-2)*

Unyenyekevu (khushui) katika swala hupatikana kwa:

1. Kutuliza mwili wakati wa kuswali.
2. Kutuliza moyo na fikra yaani mtu asifikiri chochote nje ya swala.
3. Kuzingatia yale unayosoma katika swala.
4. Kujua tafsiri ya yale unayosoma katika swala.
5. Kumzingatia Allah (s.w) na kuogopa adhabu zake.
6. Kumzingatia Allah (s.w) na kujitumainisha kwa malipo ya pepo aliyoahidi.

**Dua na Dhikri baada ya Salaam**

Mtume Muhammad (s.a.w) ametufundisha kuwa baada tu ya kutoa salaam tuseme kimya kimya:

*Astaghfirullah x 3*

Ninamuomba Allah msamaha x 3

أَسْتَغْفِرُ اللهَ

Kisha tuseme kimya kimya:

اللَّهُمَّ أَنْتَ السَّلَامُ وَمِنْكَ السَّلَامُ تَبَارَكْتَ يَاذَا الْجَلَالِ وَالإِكْرَامُ

*Allahumma Antas-Salaamu Waminkas-Salaamu Tabaarakta Yaadhiljaalia Wal-lkraami.*

Ewe Allah! Wewe ni Amani, na kwako ndiko iliko Amani. Wewe ndiye mbariki. Ee Mwenye Utukufu na Heshima.

Kisha tuseme:

سُبْحَانَ اللهِ ، الحَمْدُللهِ ، اللهُ أَكْبَرُ

*Subhaanallah x 33 (Utukufu ni wake Allah x 33 ) Al-Hamdulillah x 33 (Sifa zote anastahiki Allah x 33) , Allahu Akbar x 34, (Allah ni mkubwa kabisa x 34)*

Kisha ni vema kuleta dua yoyote, kwani dua baada ya swala ni yenye kupokelewa kwa wepesi. Ni vema kuomba dua ya Nabii Ibrahim ifuatayo:

رَبِّ ٱجْعَلْنِى مُقِيمَ ٱلصَّلَوٰةِ وَمِن ذُرِّيَّتِى ۚ رَبَّنَا وَتَقَبَّلْ دُعَآءِ ﴿٤٠﴾ رَبَّنَا ٱغْفِرْ لِى وَلِوَٰلِدَىَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ يَقُومُ ٱلْحِسَابُ ﴿٤١﴾

*Mola wangu! Nijaalie niwe msimamishaji swala, na kizazi changu (pia kiwe hivi) Mola wetu! Nakuomba upokee maombi yangu. Mola wetu! Unighufirie mimi na wazazi wangu wote wawili na wanaoamini siku ya hisabu (kiyama). (14:40-41)*

**Swala ya Jamaa**

Kwa Waislamu wanaume kuswali msikitini kwa jamaa ni lazima. Muislamu mwanamume aliyekaribu na Msikiti akiswali nyumbani pasina udhuru wa kisheria, swala yake haikubaliwi. Kwani Mtume Muhammad (s.a.w) amesema:

*Hapana swala atakayeswali mwenyewe bila ya jamaa (baada ya kusikia adhana). (Abu Daud).*

Jamaa huanza na watu wawili – Imamu (anayeswalisha) na maamuma (anayeswalishwa). Kwani Mtume (s.a.w) amesema:

*Wawili au zaidi ya hapo hufanya jamaa. (Ibn Majah).*

**Udhuru wa kutoswali jamaa**

Zifuatazo ni sababu zinazoruhusiwa Muislamu mwanamume asamehewe kuswali jamaa msikitini:

(1) Khofu ya kudhuriwa njiani.

(2) Akiwa mgonjwa.

(3) Akiwa anauguza mgonjwa.

(4) Pakiwa na mvua au jua kali sana au baridi kali sana.

**Waislamu wanawake wanaruhusiwa kuswali jamaa Msikitini**

Wanawake si lazima kwao kuswali katika jamaa Msikitini. Ni bora kwao kuswali nyumbani kama Mtume (s.a.w) anavyotufahamisha:

*Swala ya mwanamke katika nyumba yake ni bora kuliko ile atakayoswali nje ya nyumbani kwake. Na swala yake atakayoswalia chumbani mwake ni bora kuliko ile atakayoswalia sebuleni. (Abu Daud)*

Ni vizuri wanawake wakiswalia nyumbani waswali jamaa kama wako wawili au zaidi. Lakini wanawake hawakatazwi kuswali swala ya jamaa Msikitini. Kwani Mtume (s.a.w) amesema:

*Mke wa mmoja wenu atakaporuhusa ya kwenda Msikitini, huna budi kumruhusu. (Bukhari na Muslim)*

Wanawake wakitoka nyumbani kwenda Msikitini au shughuli nyingine wanatakiwa wajisitiri vizuri, wasioneshe mapambo yao na wasipake manukato. Mtume (s.a.w) anawaambia wanawake:

*Yeyote kati yenu anapokuwa Msikitini na asipake manukato. (Muslim)*

**Faida za kuswali jamaa**

Kuswali jamaa kunamsaidia mtu kuepukana na wasiwasi wa shetani wakati wa kuswali. Mtume (s.a.w) akisisitiza swala ya jamaa amesema:

> *Hawawi watu watatu katika kijiji wakaamua kuswali kila mmoja peke yake, ila shetani huwemo katika swala zao. Hapana budi kuswali jamaa kwa sababu mbwa mwitu humkamata kondoo aliyejitenga. (Ahmad, Abu Daud na Nisai)*

Hekima ya kusisitiza kuswali jamaa imeelezwa katika Hadith kuwa ni silaha ya kuunganisha nyoyo zetu na kuziwezesha kumshinda shetani, pia swala ya jamaa ina daraja au thamani kubwa zaidi ya swala ya kuswali mtu mwenyewe. Thamani yake ni mara 27 zaidi ya swala ya mtu mwenyewe. Kwani Mtume (s.a.w) amesema:

> *Swala moja inayoswaliwa katika jamaa malipo yake ni bora mara ishirini na saba (27) zaidi kuliko swala iliyoswaliwa bila jamaa. (Bukhari na Muslim).*

Kwa ujumla swala ya jamaa ina faida zifuatazo:

(1) Kuunganisha nyoyo zetu pamoja na kutuwezesha kumshinda shetani.

(2) Kutuwezesha kuwa wanyenyekevu katika swala zetu.

(3) Huimarisha udugu wa Kiislamu baina yetu kwani wenye shida hutambulika na kusaidiwa.

(4) Hutufunza kuwa watu wote ni sawa kwani tunakaa bega kwa bega katika mstari bila ya ubaguzi wowote.

(5) Hupatikana fursa ya kukumbushana wajibu wa kuamrishana mema na kukatazana mabaya.

(6) Hutufunza kuwachagua viongozi wajuzi na wacha-Mungu na kuwatii.

Hatuna budi kujihimiza kuswali jamaa ili tupate faida hizi.

**Namna ya kuswali jamaa**

Ili tupate faida za jamaa hatunabudi kuzingatia yafuatayo:

(1) Kujaza safu vizuri.

(2) Kushikamana bega kwa bega na vidole vya miguuni vishikamane.

(3) Kunyoosha mstari.

(4) Wazee na wajuzi wakae mbele karibu na Imamu.

(5) Watoto wake mstari wa nyuma.

(6) Mtu asikae mstari wa peke yake angalau wawe wawili katika mstari wa nyuma.

(7) Maamuma (anayefuata) asifanya kitendo kabla ya Imamu.

(8) Kumfuata Imamu, akisema "Allahu akbar", kimya kimya naye mamuma aseme hivyo.

(9) Imamu akisema "Samia'llahu limanhamidah", maamuma waitikie "Rabbana lakal-hamdu" kimya kimya vile vile.

(10) Kunyamaza kimya na kuzingatia wakati Imamu akisoma Suratul-Fat-ha na sura nyingine baada yake.

**Namna ya kuungana jamaa**

1. Watu wawili:



Kuna Imamu na maamuma. Maamuma hukaa pembeni kidogo upande wa kulia mwa Imamu. Hapana tofauti ya wanaume na wanawake.

2. Watu watatu:




Imamu na maamuma wawili. Kwa wanaume, Imamu hukaa mbele kiasi cha dhiraa moja (mkono mmoja uliyonyooshwa) maamuma hukaa nyuma, sawa na maamuma mwingine upande wa kulia.



Kwa wanawake, Imamu hukaa katikati mbele kidogo ya maamuma, mmoja wao hukaa kuliani na mwingine kushotoni mwake.

3. Watu wanne



Kwa wanaume, Imamu hukaa mbele kiasi cha dhiraa moja. Maamuma mmoja hukaa sawa na Imamu na wengine hukaa kushoto na kulia.

Kwa wanawake; Imamu hukaa mbali kidogo tu ya maamuma. Maamuma wawili kulia kwake na mmoja kushoto.



4. Watu zaidi ya wanne:

Kila watakaokuja wataunga mstari kulia na kushoto mpaka mstari ujae. Mara zote Imamu awe katika ya mstari. Akizidi mmoja awe upande wa kulia.



5. Mstari ukijaa:

Wanaokuja waanze mstari wa pili katikati sawa na Imamu na waujaze kulia na kushoto mpaka ujae.

6. Hairuhusiwi mtu kukaa mstari wa peke yake:

Mtume (s.a.w) alimwamuru mtu aliyeswali nyuma yake kuwa arudie swala. Ukikuta mstari umejaa na uko peke yako aliyechelewa, mguse mtu wa katikati sawa na Imamu arudi nyuma hatua moja nawe usimame kuliani kwake. Wa mstari wa mbele itabidi wasogee kujaza pengo kutokea kushoto.

**Zakat**

Kutoa Zakat ni nguzo ya tatu ya Uislamu.

Zakat ni sehemu ya mali ya tajiri anayoitoa kumpa Muislamu aliye Masikini au wengineo walioorodheshwa katika Qur-an. Zakat hutolewa kila baada ya mwaka au baada ya mavuno. Mtume (s.a.w) amesema:

> *Nimeamrishwa nichukue Zakat kutoka kwa matajiri miongoni mwenu na nigawanye kwa masikini miongoni mwenu.*

### Aina za mali zinazotolewa Zakat

Muislamu akimiliki mali kadhaa hulazimika kuitolea Zakat. Aina za mali zinazotolewa Zakat ni zifuatazo:

(1) Dhahabu.

(2) Vito vya dhahabu au mapambo ya dhahabu.

(3) Madini ya fedha na mapambo yake.

(4) Fedha taslimu (hela).

(5) Mali ya biashara.

(6) Mifugo – ngamia, ng'ombe, mbuzi na kondoo.

(7) Mazao ya shambani.

(8) Mali iliyochimbuliwa chini kama vile madini.

### Wanaostahiki kupewa Zakat

Wanaostahiki kupewa Zakat wameorodheshwa katika Qur-an katika aya ifuatayo:

إِنَّمَا ٱلصَّدَقَٰتُ لِلْفُقَرَآءِ وَٱلْمَسَٰكِينِ وَٱلْعَٰمِلِينَ
عَلَيْهَا وَٱلْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِى ٱلرِّقَابِ وَٱلْغَٰرِمِينَ وَفِى
سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱبْنِ ٱلسَّبِيلِ ۖ فَرِيضَةً مِّنَ ٱللَّهِ ۗ وَٱللَّهُ
عَلِيمٌ حَكِيمٌ ۝

*Sadaka (Zakat) hupewa watu hawa: Mafakiri, masikini, wanaozitumikia, wanaotiwa nguvu nyoyo zao (juu ya Uislamu), katika kuwakomboa watumwa, katika kuwasaidia wenye deni, katika njia ya Mwenyezi Mungu na katika kuwapa wasafiri (walioharibikiwa). Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye Hikima. (9:60).*

Kutokana na aya hii, wanaostahiki kupewa Zakat na sadaqa ni hawa wafuatao:

(1) Mafukara: Wale wasiojiweza kabisa, masikini hohe hahe.

(2) Masikini: wale wanaojiweza kidogo, lakini hawana uwezo wa kutosheleza mahitaji yao ya maisha.

(3) Wanaozitumikia: Wakusanyaji na wagawaji wa Zakat.

(4) Wanaotiwa nguvu nyoyo zao: Wale waliosilimu hivi karibuni.

(5) Katika kuwakomboa watumwa.

(6) Kuwasaidia wenye madeni kulipa madeni yao.

(7) Katika njia ya Allah: Yaani kwa ajili ya maendeleo ya Uislamu kwa ujumla na katika kupigania dini ya Allah.

(8) Kuwapa wasafiri walioharibikiwa.

## Funga ya Ramadhani

Waislamu wameamrishwa kufunga Ramadhani katika aya ifuatayo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُتِبَ عَلَيْكُمُ ٱلصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ
عَلَى ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿١٨٣﴾

*Enyi mlioamini! Mumelazimishwa (mumeamrishwa) kufunga kama walivyoamrishwa waliokuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mwenyezi Mungu. (2:183)*

## Maana ya kufunga (Swaumu)

Kufunga ni kujizuilia kula, kunywa, kuvuta sigara, kuingiza chochote puani au masikioni pamoja na kujizuilia kufanya mambo maovu katika mchana mzima kuanzia alfajiri mpaka magharibi.

**Wanaolazimika kufunga**

Waislamu wote wanalazimika kufunga mwezi wa ramadhani. Watoto wakifikia umri wa miaka saba waanze kuzoeshwa kufunga na wakifikia umri wa miaka 10 walazimishwe kufunga.

**Wanaosamehewa kufunga Ramadhani**

Wafuatao wamesamehewa kufunga:

(1) Watoto wadogo chini ya umri wa miaka saba.

(2) Wazee vikongwe.

(3) Wagonjwa lakini wakipona walipe siku walizoacha kufunga.

(4) Wasafiri lakini baada ya ramadhani watalipa siku walizokula wakiwa safarini.

**Kuanza na kumalizika mwezi wa Ramadhani**

Ramadhani huanza kwa kuandama mwezi na huisha kwa kuandama mwezi wa shawwal baada ya siku 29 au 30. Waislamu wakipata habari ya uhakika ya kuandama mwezi popote pale ulimwenguni wanalazimika kuanza kufunga ramadhani au kufungua na kuswali Idd.

**Nguzo za funga**

Ili funga ikamilike mfungaji hana budi kutekeleza nguzo zifuatazo:

(1) Kutia nia ya kufunga kabla ya alfajiri. Hapana maneno maalumu ya kusema bali Muislamu hutia nia moyoni mwake na kudhamiria kuwa atafunga siku inayofuata. Mwisho wa kutia nia ni mwisho wa daku.

(2) Kujizuilia kula, kunywa, kuvuta sigara, kuingiza chochote kwenye pua na masikio, kujizuia kusema uongo, kusengenya, kugombana na kujizuilia kufanya uovu wowote.

**Yanayobatilisha funga**

Mwenye kufunga akifanya mojawapo katika haya yafuatayo swaumu yake itakuwa imeharibika;

(1) Kula, kunywa, kuvuta sigara, na kuingiza kitu puani au masikioni makusudi.

(2) Kusema uwongo, kusengenya au kufanya uovu wowote makusudi, kwani imepokelewa kwa abu Hurairah kuwa Mtume wa Allah amesema:

> *Yeyote yule ambaye hataacha mazungumzo mabaya na vitendo viovu, Allah (s.w) hana haja na kuacha kwake chakula chake na kinywaji chake. (Bukhari).*

**Yasiyobatilisha funga**

Yafuatayo hayabatilishi funga:

(1) Kula au kunywa kwa kusahau.

(2) Kuoga.

(3) Kupiga mswaki.

(4) Kusukutua na kupandiliza maji puani wakati wa kutawadha lakini maji yasiingie ndani.

(5) Kutia dawa machoni.

(6) Kupiga sindano.

(7) Kupaka mafuta.



## Zoezi la Tatu

1. Twahara ni…………………………………………………………
2. Tayammamu maana yake ni………………...…………………..
3. Tafuta udongo safi kisha onesha kwa vitendo namna ya kutayamamu hatua kwa hatua.
4. Taja mambo matatu muhimu yanayokamilisha swala
5. Bainisha nguzo za swala zinazopatikana katika mafungu matatu yafuatayo:

    (a) Nguzo ya moyoni

    (b) Nguzo za matamshi au kisomo

    (c) Nguzo za matendo
6. Taja tafauti tatu zilizopo baina ya sijidatis-sahau na sijidat-tilaawat.
7. Bainisha faida za waislamu kuswali jamaa msikitini.
8. Nini tofauti kati ya zakkat na swaumu?
9. Orodhesha mambo ya kufanya ili uwe na khushui katika swala.

# Somo la 4. Akhlaq

## UTAMADUNI WA KIISLAMU

### VAZI LENYE SITARA

Vazi lenye sitara ni katika utamaduni wa kiislamu unaomtambulisha muislamu katika jamii. Vazi lenye sitara hufunika uchi na huhifadhi mwili wa mwanadamu, na kuupa hadhi yenye heshima kubwa kuliko wanyama. Kuvaa vazi lenye sitara ndiyo utu na ndiyo jambo la asili kama tunavyojifunza katika Qur-an:

يَٰبَنِيٓ ءَادَمَ قَدۡ أَنزَلۡنَا عَلَيۡكُمۡ لِبَاسٗا يُوَٰرِي سَوۡءَٰتِكُمۡ وَرِيشٗاۖ
وَلِبَاسُ ٱلتَّقۡوَىٰ ذَٰلِكَ خَيۡرٞۚ ذَٰلِكَ مِنۡ ءَايَٰتِ ٱللَّهِ لَعَلَّهُمۡ
يَذَّكَّرُونَ ٢٦

*Enyi wanaadamu! Hakika tumekuteremshieni nguo zifichazo tupu zenu na nguo za pambo, na nguo za ucha Mungu ndizo bora. Hayo ni katika ishara za Mwenyezi Mungu ili mpate kukumbuka. (7:26)*

Aya hii inatufahamisha kuwa Allah (s.w) amewafanya wanaadamu wavae nguo, wasikae uchi kama wanyama. Kisha akawapa elimu ya kutengeneza nguo. Kisha aya hii Allah (s.w) anabainisha wazi kuwa; kusudio la nguo ni kusitiri uchi na kuwa pambo. Aya inasisitiza kuwa nguo za ucha Mungu ndizo bora.

Nguzo za ucha Mungu ni zile zinazovaliwa kwa kuchunga mipaka ya mavazi aliyotuwekea Allah (s.w) kama wanawake na wanaume.

**(i) Mipaka ya mavazi kwa wanawake wa Kiislamu**

Mipaka ya mavazi ya wanawake wa Kiislamu imebainishwa katika aya zifuatazo:

وَقُل لِّلْمُؤْمِنَٰتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَٰرِهِنَّ وَيَحْفَظْنَ
فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا ۖ
وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ جُيُوبِهِنَّ ۖ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ

*Na waambie Waislamu wanawake wainamishe macho yao na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe viungo vyao isipokuwa vinavyodhihirika (navyo ni uso, viganja na nyayo) na waangushe shungi zao mpaka vifuani mwao na wasionyeshe mapambo yao. (24:31)*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِيُّ قُل لِّأَزْوَٰجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَآءِ ٱلْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ
عَلَيْهِنَّ مِن جَلَٰبِيبِهِنَّ ۚ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰٓ أَن يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَيْنَ ۗ وَكَانَ
ٱللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ۝

*Ewe Mtume! Waambie wake zako, na binti zako na wanawake wa Kiislamu (wengine) wajiteremshie vizuri nguo zao. Kufanya hivyo kutawapelekea upesi wajulikane kuwa ni watu wa heshima ili wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe mwingi wa kurehemu. (33:59)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa:

(i) Wanawake wanalazimika kujifunika mwili mzima isipokuwa uso, vitanga vya mikono na nyayo.

(ii) Shungi ishuke mpaka kifuani huku ikiwa imefunika magega. Vitambaa vinavyofunika tu kichwa havikamilishi hijabu.

(iii) Nguo isiwe yenye kubana. Iwe pana.


(iv) Nguo isiwe ni yenye kuonyesha.

(v) Nguo isiwe na mapambo yenye mvuto mkali. Wala nguo zisivaliwe ili kuwakoga wengine. Maringo, majivuno na kujikweza ni vipengele vya tabia vilivyoharamishwa katika Uislamu.

(vi) Nguo ya mwanamke isiwe sawa na ile ya kiume. Kwa mfano ni haramu kwa mwanamke kuvaa shati na suruali. Bali mwanamke anaruhusiwa kuvaa kanzu (gauni) na suruali ndani.

(vii) Mwanamke wa Kiislamu asiige mitindo ya mavazi ya wasiokuwa Waislamu. Kwa mfano ni haramu kuiga kuvaa "kepu" na shela wakati wa arusi. Ni haramu kufanya hivyo hata kama vazi hilo linatimiza masharti mengine ya Hijab.

(viii) Mwanamke wa Kiislamu anaruhusiwa kujipamba kwa kuvaa hereni, mkufu, bangili na mapambo mengine lakini asiyadhihirishe kwa kuyaweka wazi au kujitingisha. Vile vile mwanamke wa Kiislamu amekatazwa kupaka manukato yenye harufu kali.




**(ii) Mipaka ya mavazi kwa wanaume wa Kiislamu**

Kwa mtazamo wa Uislamu uchi wa mwanaume ni sehemu yote iliyo kati ya kitovu na magoti. Hivyo ni haramu kwa Muislamu kuvaa kaptura, bukta au taulo inayoacha wazi sehemu hiyo kati ya kitovu na magoti hadharani. Kwa kuzingatia mipaka ya uchi wa mwanaume, tunajifunza mipaka ya vazi la mwanaume wa Kiislamu kuwa:

(i) Muislamu asivae vazi linaloacha wazi sehemu yoyote iliyo kati ya kitovu na magoti.





(ii) Muislamu mwanaume asivae vazi la kike au kuvaa mapambo kama vile bangili, vidani, hereni, mkufu. Pia ni haramu kusuka nywele kama wafanyavyo wanawake.

(iii) Muislamu asiige mitindo ya mavazi ya wasiokuwa Waislamu. Kwa mfano kuvaa nguo zenye misalaba, kuigiza mitindo ya kihuni.

(iv) Nguo ya Muislamu isiwe yenye kuburuza chini.

(v) Muislamu mwanaume haruhusiwi kuvaa vazi la hariri. Hili ni vazi litakalovaliwa na watu wa Peponi tu. Mtume (s.a.w) amewakataza Waislamu vazi hili kama tunavyojifunza katika hadithi ifuatayo:

> *Ibn Omar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hakika yule anayevaa vazi la hariri katika maisha haya ya dunia, hatakuwa na kasma (sehemu) katika maisha ya akhera. (Bukhari na Muslim).*

(vi) Muislamu asivae vazi linalompelekea kujivuna na kujisikia.

(vii) Ni sunnah kuvaa nguo nyeupe hasa wakati wa kwenda Msikitini kama tunavyojifunza katika hadithi ifuatayo:

> *Abuu Darda'a ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hakika vazi lililo bora kuvaa katika kukutana na Allah katika kaburi lako au msikitini ni jeupe. (Ibn Majah)*

Pia Mtume (s.a.w) anahimiza vazi jeupe katika hadith ifuatayo:

> *Samurah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Vaa vazi jeupe kwa sababu ni safi kuliko yote na litumieni kwa sanda kwa ajili ya maiti zenu". (Ibn Majah, Ahmad, Tirmidh, Nisai)*

Pia Mtume (s.a.w) alipendelea sana vazi la kanzu kama tunavyojifunza katika Hadith:

> *Ummu salamah ameeleza kuwa vazi alilokuwa akilipenda Mtume wa Allah ni kanzu. (Tirmidh, Abu Daud).*

**Faida ya Kuvaa Hijab**

Mwanamke wa Kiislamu anapojisitiri kwa kuchunga mipaka ya Allah (s.w) hupata hadhi na heshima inayomstahiki. Hivi ndivyo Allah (s.w) anavyotufahamisha katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِىُّ قُل لِّأَزْوَٰجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَآءِ ٱلْمُؤْمِنِينَ يُدْنِينَ
عَلَيْهِنَّ مِن جَلَٰبِيبِهِنَّ ۚ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰٓ أَن يُعْرَفْنَ فَلَا يُؤْذَيْنَ ۗ وَكَانَ
ٱللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٥٩﴾

> *Ewe Mtume! Waambie wake zako, binti zako, na wanawake wa Kiislamu (wengine – waambie), wajiteremshie uzuri nguo zao. Kufanya hivyo kutapelekea upesi wajulikane (kuwa ni watu wa hishima ili) wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusemehe (na) Mwingi wa kurehemu. (33:59)*

**Kuwa na haya**

Waislamu wanatakiwa wawe na haya. Waone haya kukaa uchi. Pia waone haya kuwa na tabia chafu. Iwe ni aibu kwa Muislamu kuwa nje ya vazi la sitara. Pia iwe ni aibu kwa Muislamu kuwa na tabia chafu. Kuwa na haya ni dalili ya kuwa na imani kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: “Haya ni sehemu ya imani na imani sehemu yake ni peponi, ukosefu wa haya ni sehemu ya ugumu wa moyo, na ugumu wa moyo mahali pake ni motoni”. (Ahmad, Tirmidh)

**Michezo katika Uislamu**

Michezo katika Uislamu inaruhusiwa kwa lengo la kupata faida zifuatazo:

(i) Kuuchangamsha mwili na kuufanya uwe mwepesi.

(ii) Kuchangamsha akili na kuondoa ugoigoi.

(iii) Kuufanya mwili uwe na nguvu na staha nzuri.

(iv) Kumpa muumini mazoezi ya ukakamavu na shabaha ili kuwa tayari kupambana na adui wakati wowote. Kila Muislamu ni askari wa kupigania dini ya Allah.

**Ili kupafa faida hizi, michezo ifuatayo inaruhusiwa:**

(i) Michezo yote ya riadha, kama vile mbio, kuruka, kutupa vitu, kuogolea, mpira wa mikono, mpira wa miguu nakadhalika.

(ii) Michezo yote ya kupimbana nguvu, kama vile kuvutana, mielekea, kareti na judo.

(iii) Michezo yote ya kulenga shabaha.

(iv) Michezo yote inayofundisha mbinu za kivita

(v) Michezo yote ya mazoezi ya viungo na ukakamavu

**Miiko ya kuchunga wakati wa kucheza**

Waislamu hasa vijana wanatakiwa wajihimize kushiriki katika michezo hiyo iliyotajwa lakini kwa kuchunga miiko ifuatayo:

(i) Wacheze katika muda na mahali maalumu palipotengwa kwa ajili hiyo. Wasicheze ovyo-ovyo njiani na wakati wowote.

(ii) Wasitumie muda mrefu katika michezo. Muda wa nusu saa hadi saa moja kulingana na aina ya mchezo unaochezwa unatosha kabisa kwa mazoezi na michezo ya kawaida. Mchezo usipitishe zaidi ya masaa mawili mfululizo.

(iii) Wakati wa kucheza mipaka ya Allah (s.w) izingatiwe, mavazi yawe ya stara, isitumike lugha chafu, upenzi usiwe wa kupindukia n.k.

**Michezo iliyoharamishwa katika Uislamu**

Qur-an imeharamisha michezo ya kikamari katika aya ifuatayo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِنَّمَا ٱلْخَمْرُ وَٱلْمَيْسِرُ وَٱلْأَنصَابُ وَٱلْأَزْلَٰمُ
رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ ٱلشَّيْطَٰنِ فَٱجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾

*Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (na kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kutazamia mishare ya kupigia ramli (yote haya) ni uchafu (ni) katika kazi za Shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu (kutengenekewa). (5:90)*

Pia katika hadith ibn Umar ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) ameharamisha ulevi (mvinyo), michezo ya kamari, ngoma na aina nyingine ya pombe… (Abu Daud)

Katika Qur-an na hadith tunajifunza kuwa michezo iliyoharamishwa katika Uislamu ni hii ifuatayo:

(i) Michezo yote inayoambatana na ulevi.

(ii) Michezo yote ya pata potea kama vile kamari,bingo, karata, fete fete, tombola, chess, gololi, bao, nakadhalika.

(iii) Michezo yote ya ngoma kama vile mdundiko, disko, dansi nakadhalika.

(iv) Nyimbo na mashairi yanayompelekea mtu kuchupa mipaka ya Allah (s.w).

(v) Michezo yote inayopoteza muda na kumpumbaza mtu kiasi cha kumsahaulisha lengo la kuumbwa kwake. Hii ni michezo ya Laghwi. Sababu ya kukatazwa kwa michezo hii inabainishwa katika aya zifuatazo:

يَسْـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلْخَمْرِ وَٱلْمَيْسِرِ ۖ قُلْ فِيهِمَآ إِثْمٌ
كَبِيرٌ وَمَنَٰفِعُ لِلنَّاسِ وَإِثْمُهُمَآ أَكْبَرُ مِن نَّفْعِهِمَا ۗ

*Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari. Sema, katika hivyo mna madhara makubwa na (baadhi ya) manufaa kwa (baadhi ya) watu. Lakini madhara yake ni makubwa zaidi kuliko manufaa yake… (2:219)*

إِنَّمَا يُرِيدُ ٱلشَّيْطَٰنُ أَن يُوقِعَ بَيْنَكُمُ ٱلْعَدَٰوَةَ وَٱلْبَغْضَآءَ
فِى ٱلْخَمْرِ وَٱلْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَن ذِكْرِ ٱللَّهِ وَعَنِ ٱلصَّلَوٰةِ ۖ فَهَلْ
أَنتُم مُّنتَهُونَ ﴿٩١﴾

*Hakika Shetani anataka kukutilieni uadui na bughudha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari na anataka kukuzuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na (kukuzuilieni) kuswali. Basi je, hamtaacha (mabaya hayo). (5:91)*

Kutokana na aya hizi tunajifunza kuwa sababu za kuharamishwa michezo hiyo ni hizi zifuatazo:

(i) Husababisha uadui na bughudha. Kwa mfano katika michezo ya kamari tuliyoitaja kuna kudhulumiana, kuhusudiana, kudharauliana, kusengenyana, uongo, kupigana na yale yote yanayosababisha uadui na bughudha baina ya watu.

(ii) Kupoteza muda mwingi sana ambao ungetumika kweye shughuli zenye kuleta manufaa kwa watu.

(iii) Kupoteza nguvu nyingi sana ambazo zingetumika kwa shughuli

zenye kuleta manufa kwa watu. Kwa mfano wachezaji wa ngumi, hutumia nguvu nyingi sana badala ya kutumia nguvu hizo kwenye kazi viwandani, mashambani, n.k.

(iv) Huwafanya wachezaji, wasikilizaji na watazamaji wasahau kumkumbuka Mwenyezi Mungu na Shetani huwa mpambe wao. Muislamu anatakiwa muda wote awe anamkumbuka Mwenyezi Mungu.

(v) Huwazuilia Waislamu kuswali kwa wakati makhsusi uliowekwa kwa kila swala. Mara nyingi michezo hii huwasahaulisha Waislamu kuswali. Kutokana na sababu hizi, hata kama michezo hii itaonekana yenye faida machoni mwa watu, kwa waumini ina madhara na hasara kubwa.

**Michezo ya Laghwi**

Michezo ya laghwi ni aina zote za michezo inayowapumbaza watu kiasi cha kuwasahaulisha lengo la kuumbwa kwao. Tumeumbwa ili tumuabudu Allah (s.w) kwa muda wote wa saa 24 za siku. Yaani tunatakiwa tuishi kwa kuwajibika kwa Allah (s.w) kwa kutekelza maamrisho yake yote na kujiepusha na makatazo yake yote. Kila wakati tunatakiwa tuwajibike kwa Allah (s.w) kiasi hicho. Jambo lolote litakalomtoa Muislamu katika kumkumbuka na kumtumikia Allah (s.w) litakuwa ni haramu. Waumini wa kweli ni wale wenye sifa ya kujiepusha na laghwi (mambo ya upuuzi) kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ ﴿٢﴾

وَالَّذِينَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾

*Hakika wamefuzu waumini ambao katika swala zao huwa wanyenyekevu. Na ambao hujiepusha na laghwi (mambo ya upuuzi). (23:1-3)*



## Zoezi la Nne

1. Taja mavazi manne yavaliwayo hadharani ambayo si sitara.

    (a)..........................................................

    (b)..........................................................

    (c)..........................................................

    (b)..........................................................

2. Orodhesha faida tano za kuvaa hijabu

    (a)..........................................................

    (b)..........................................................

    (c)..........................................................

    (b)..........................................................

    (e)..........................................................

3. Taja michezo ambayo mtu akishiriki hupata dhambi.

4. Taja mambo muhimu ya kuzingatiwa katika michezo.

5. Nini maana ya *Laghwi*

6. Kwanini ni muhimu muislamu kushiriki michezo?

7. Taja michezo ambayo mtu akishiriki hupata thawabu.

# UISLAMU WAKATI WA MTUME (S.A.W)

## KUANZISHA DOLA YA KIISLAMU MADINAH

Mwenyezi Mungu ametufahamisha katika Qur-an kuwa lazima tufuate maagizo yake katika kila jambo tunalolifanya kwa sababu Yeye ndiye aliyetuumba sisi na kila kitu katika ulimwengu huu na kwa hiyo Yeye peke yake ndiye mwenye mamlaka ya kutuhukumu. Na ni Mwenyezi Mungu peke yake aliye na haki ya kuhukumu jambo lipi ni halali na jambo lipi ni haramu. Na hata Mitume hufuata yale tu walioteremshiwa kutoka kwa Mwenyezi Mungu, hawatungi hukumu zao kwa matashi yao binafsi.



Lengo la Mtume (s.a.w) kuhamia Madinah lilikuwa ni kutafuta mazingira mazuri yatakayowawezesha Waislamu kufuata hukumu za Mwenyezi Mungu katika kila jambo wanalolifanya. Mazingira hayo yalipatikana baada ya Waislamu wa Madinah kuchukua ahadi ya kuwapokea ndugu zao wa Makkah na kusaidiana nao katika kuusimamisha Uislamu. Kwa kuwa Muhammad (s.a.w) alikuwa ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, yeye ndiye aliyekuwa kiongozi wa kuwaelekeza Waislamu kwa vitendo namna ya kuijenga jamii kwa misingi ya Kiislamu. Na mara tu baada ya kufika Madinah Mtume (s.a.w) alifanya mambo ya msingi yafuatayo:

(i) Alianzisha ujenzi wa Msikiti wa Qubah.

(ii) Aliujenga Msikiti wa Madinah na kuutumia kama kituo cha Dola.

(iii) Aliunganisha udugu baina ya Answari na Muhajirina.

(iv) Aliiandika katiba ya Madinah.

**Msikiti wa Qubah**

Mtume (s.a.w) alipoingia Madinah alijipumzisha kwenye kitongoji cha Qubah kwa muda wa siku chache. Katika siku ya pili ya kukaa kwake hapo Qubah Mtume (s.a.w) aliamuru ujengwe msikiti. Mtume mwenyewe alishiriki katika kuujenga Msikiti huu wa kwanza katika mji wa Madinah. Aliwaachia Waislamu wa pale kuumalizia alipoondoka kuelekea kwenye kituo kilichokusudiwa kuwa makazi yake na kituo cha Dola atakayoianzisha. Msikiti wa Qubah umetajwa katika Qur-an (9:108) pale Mwenyezi Mungu aliposema:

لَّمَسْجِدٌ أُسِّسَ عَلَى ٱلتَّقْوَىٰ مِنْ أَوَّلِ يَوْمٍ أَحَقُّ أَن تَقُومَ
فِيهِ ۚ فِيهِ رِجَالٌ يُحِبُّونَ أَن يَتَطَهَّرُوا۟ ۚ وَٱللَّهُ يُحِبُّ
ٱلْمُطَّهِّرِينَ ﴿١٠٨﴾

*… Msikiti uliojengwa juu ya msingi wa ucha Mungu tangu siku ya kwanza (ya kufika Mtume Madinah) unastahiki zaidi wewe usimame humo. Humo wamo watu wanaopenda kujitakasa. Na Mwenyezi Mungu anawapenda wajitakasao. (9:108)*

Ujenzi wa Msikiti kuwa ndio jambo la kwanza alilolifanya Mtume (s.a.w) mara tu baada ya kuhamia Madinah, kunatupa fundisho kuwa Msikiti ni kitu muhimu sana katika kuuhuisha na kuuendeleza Uislamu.

**Msikiti Mkuu wa Madinah**

Mara tu baada ya kuwasili kwenye sehemu aliyoelekezwa na Mola wake, Mtume (s.a.w) aliamuru eneo la sehemu ile linunuliwe kwa ajili ya Msikiti na makazi yake. Kazi ya ujenzi wa Msikiti wa Madinah ulioitwa “Msikiti Mtume” ilianza

kwa hima kubwa na Waislamu wote walishiriki. Mtume mwenyewe alishiriki katika ujenzi huu sawa na Waislamu wengine na wakati mwingine aliwazidi kwa kubeba mawe yaliyoshindikana kwa uzito. Waislamu walijihamasisha katika kazi kwa kaswida (nyimbo) na Mtume mwenyewe aliungana nao katika kuiimba kaswida ifuatayo:

*"Ee Allah Kufuzu pekee ni kufuzu katika maisha ya Akhera.*
*Kwa hiyo wasamehe Muhajirina na Answaari".*

Msikiti wa Mtume ulijengwa kwa matofali mabichi, yaani yasiyochomwa, ulipauliwa kwa boriti za mitende na kuezekwa kwa makuti ya mitende, na haukuwa na alama ya Qibla. Hapakuwa na mapambo yoyote ndani au nje ya msikiti huo. Ulikuwa ni msikiti wa kawaida uliojengwa kwa gharama ndogo.

Msikiti wa Mtume haukuwa na sehemu ya kuswalia peke yake, bali ulitumika pia kwa shughuli nyingi nyinginezo kama ifuatayo:

**(i)Mahali pa kuswalia swala za jamaa**

Sehemu ya kukutana kwa ajili ya swala tano za jamaa pamoja na Ijumaa. Imamu wa msitiki huu alikuwa Mtume(s.a.w).

**(ii)Kituo cha mafunzo**

Mtume (s.a.w) aliwafundisha watu Uislamu ndani ya Msikiti wake. Pia Msikiti ulitumika kama mahali pa kufundishana (kusomeshana).

**(iii)Maktaba**

Msikiti ulitumika pia kama mahali pa utulivu pa kujisomea.

**(iv)Ikulu ya Mtume**

Shughuli zote za uongozi wa dola zilifanyika msikitini.

**(v)Mahakama**

Pia msikiti ulitumika kama mahakama ambapo kesi ziliendeshwa na kupewa haki yake, kila aliyedhulumiwa na kupewa adhabu inayostahiki kwa kila mkosaji.

**(vi)Bunge (Majlis Shura)**

Wakati wa Mtume (s.a.w) mijadala na mashauriano yote juu ya uendeshaji wa dola ya Kiislamu yalifanyika Msikitini.

**(vii)Kituo cha mikutano**

Ilipotokezea haja ya kukutana wakati wowote ule nje ya nyakati za swala za jamaa, Waislamu walikutania msikitini. Walikuwa wakiitana kwa adhana maalum isiyokuwa na "Hayya 'ala Swalah" wala "Hayya 'Alal-Falah"

**(viii)Kituo cha Kijeshi**

Wakati wa Mtume (s.a.w) msikiti pia ulitumika kama kituo cha jeshi. Mtume (s.a.w) alikuwa ndiye Amiri Jeshi Mkuu wa jeshi la Kiislamu, na hiyo aliwaita Waislamu msikitini na kutoa amri za kijeshi kila ilipotokea haja ya kufanya hivyo.

**(ix)Nyumba ya kulala wageni**

Katika kona ya misikiti wa Mtume (s.a.w) palitengwa sehemu ya kulala wageni na maskini wasiojiweza waliojulikana kwa jina la as-hab Suffah.

Kutokana na ujenzi wa msikiti wa Mtume (s.a.w) na matumizi yake tunajifunza kuwa:

(i) Msikiti ni kituo muhimu katika harakati za kuuhuisha na kuuendeleza Uislamu.

(ii) Uislamu ni utaratibu wa maisha. Unajihusisha na kila kipengele cha maisha kinachowahusu watu binafsi na jamii yao. Uislamu unajihusisha na uchumi, siasa, utamaduni, nakadhalika, kama tunavyojihusisha na swala.

**Kuunganisha Udugu**

Waarabu wa Yathrib waligawanyika katika makabila makubwa mawili ambayo ni Aus na Khazraj. Makabila haya yalichukiana na yalikuwa yakipigana mara kwa mara. Baada ya watu wa makabila haya kusilimu waliishi kindugu chini ya uongozi wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Waislamu hawa wa Madinah kwa umoja wao walijulikana kwa jila la Answaari, yaani wenye kuwanusuru Waislamu waliohamia Madinah kutoka Makkah.

Kwa upande mwingine Waarabu wa Makkah nao waliganyika katika koo mbali mbali. Kila mmoja aliuona ukoo wake kuwa bora kuliko wa mwingine. Waislamu wa Makkah chini ya uongozi wa Mtume Muhammad (s.a.w) walishikamana pamoja kuzitupilia mbali tofauti za kiukoo na kikabila. Waislamu wa Makkah walipohamia Madinah kwa umoja walijulikana kwa jina la Muhajirina, yaani waliohamia Madinah kutoka Makkah.

Mtume (s.a.w) kwa maelekezo ya Mola wake alifanya jambo la kuwaunganisha Waislamu kutoka Makkah na wale wenyeji wao wa Madinah. Mtume (s.a.w) aliunganisha udugu baina ya answaari na Muhajiriina.

Udugu huu ulikuwa na nguvu zaidi kuliko ule udugu wa kawaida wa nasaba. Udugu huu ulitatua tatizo la kiuchumi la wale wageni. Udugu huu pia ulizidisha mshikamano wa Waislamu na hivyo kuimarisha nguvu zao kiuchumi na kijeshi. Kutokana na tukio hilo la kihistoria la Mtume kuwaunganisha Waislamu tunajifunza yafuatayo:

(i) Umoja na mshikamano wa Waislamu ni jambo la awali la msingi katika kusimamisha Dola ya Kiislamu.

(ii) Mshikamano wa Waislamu ndio zana pekee itakayowapa nguvu za kiuchumi na za kijeshi.

(iii) Udugu wa Kiislamu ndiyo udugu hasa mzito zaidi ya ule wa nasaba, kabila ukoo, au taifa. Kwa sababu ya umuhimu wa jambo hili, Qur-an inatuhimiza kushikamana katika aya zifuatazo:

وَٱعْتَصِمُوا۟ بِحَبْلِ ٱللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا۟

*Na shikamaneni kwa kamba (dini) ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane. (3:103)*

إِنَّمَا ٱلْمُؤْمِنُونَ إِخْوَةٌ فَأَصْلِحُوا۟ بَيْنَ أَخَوَيْكُمْ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ
لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ١٠

*Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu, basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na mcheni Mwenyezi Mungu ili mrehemewe. (49:10)*

## Mkataba wa Madinah

Baada ya Mtume (s.a.w) kuwaunganisha Waislamu kuwa umma mmoja alichukua hatua ya kuwaunganisha watu wote wa mji wa Madinah bila kujali dini zao. Palikuwepo Wayahudi waliodai kumfuata Nabii Musa (a.s). Mtume (s.a.w) aliwaendea Wayahudi na kuwafahamisha kuwa yeye ni Mtume wa Allah kama Mitume wengine waliomtangulia. Aliwafahamisha kuwa yeye amekuja kuthibitisha dini ya Mitume hao na sio kuwapinga. Pia aliwathibitishia kuwa yeye ni Mtume aliyeletwa kupitia kwa Waarabu kama ambavyo Nabii Mussa (a.s) alivyoletwa kupitia kwa wana wa Israeli.

Mtume (s.a.w) aliandika mkataba wa Madinah uliofafanua vizuri nafasi, haki na wajibu wa kila watu katika dola. Sehemu ya kwanza ya mkataba iliwahusu Waislamu. Ilibainisha wazi kuwa Waislamu wote ni umma mmoja bila ya kujali tofauti zao za kiukoo, kikabila, kitaifa n.k. Mkataba huo pia ulifafanua wazi kuwa Muhammad (s.a.w) ndiye kiongozi na msemaji mkuu wa masuala yote yanayowahusu Waislamu. Yaani Waislamu wote waliwajibika kumtii Mtume (s.a.w) na kuufuata mwongozo wake katika masuala yote yanayohusu maisha yao.

Sehemu ya pili ya mkataba huu iliwahusu Wayahudi na Waarabu waliokuwa hawajasilimu bado. Iliweka msingi wa mahusiano baina ya Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Chini ya mkataba huu kila mtu alikuwa na uhuru kamili wa kutoa mawazo yake na kuabudu atakavyo. Kila mkazi wa Madinah bila ya kujali dini yake alikuwa na haki ya kulindwa uhai wake na mali yake. Uovu na udhalimu wa kila aina ulipigwa marukufu. Mkataba huu pia ulitamka wazi kuwa Muhammad (s.a.w) ndiye kiongozi na Amiri Jeshi Mkuu.

## Mkataba baina ya Mtume (s.a.w) na makabila ya pembezoni

Makabila yaliyokuwa pembezoni mwa mji wa Madinah yahakuhusika na "mkataba wa Madinah". Makabila ya Kiyahudi yaliyoishi pembezoni mwa mji huo wa Madinah ni Banu Quraizah, Banu Nadhir na Banu Qainuqa.Kutokana na mkataba huo wa Madinah tunajifunza mambo makuu yafuatayo:

(i) Kuingia katika Uislamu ni hiari ya mtu na sio kazi ya dola ya Kiislamu kuwalazimisha watu kuwa Waislamu.

(ii) Kazi ya Dola ya Kiislamu ni kuhakikisha kuwa kila mtu anakuwa huru kufuata dini yake.

(iii) Kazi nyingine muhimu ya dola ya Kiislamu ni kuhakikisha kuwa kila mtu anapata haki zake katika jamii, mahitaji ya msingi na pia kudumisha amani na utulivu.

## Kutokeza kwa kundi la Wanafiki

Baada ya Mtume (s.a.w) kuhamia Madinah haukupita muda mrefu watu karibu wote, isipokuwa Wayahudi walisilimu. Lakini siyo watu wote waliosilimu kikwelikweli. Wapo wale ambao walisema kuwa wamesilimu na kumbe katika nafsi zao hawakuridhia kuwa Waislamu. Watu hawa waliongozwa na Abdullah bin Ubay, ambaye muda mfupi kabla ya Mtume (s.a.w) kuhamia Madinah alikuwa avishwe taji la kuwa mfalme wa Madinah. Mpango huo ulisitishwa baada ya kuja Mjumbe wa Allah. Na hivyo katika moyo wake Abdullah bin ubay alimchukia sana Mtume na hivyo akawa mstari wa mbele katika kuupiga vita Uislamu kichinichini. Kundi hili la wanafiki lilishirikiana na maadui wengine wa nje katika kuupiga vita Uislamu.

## Mabadiliko ya Qibla na athari zake

Mwanzo kabisa Waislamu walipokuwa wakiswali walikuwa wakielekea Baitil Muqaddas, Yerusalemu. Wayahudi pia walikuwa wakielekea huko katika Ibada zao. Lakini ilipofika mwezi wa Rajab, katika mwaka wa 2 A.H. Mwenyezi Mungu aliwaamuru Waislamu wanaposwali waelekee Baitul-haram, Makkah aliposema katika Qur-an:

فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ ۚ وَحَيْثُ مَا كُنتُمْ
فَوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُۥ ۗ وَإِنَّ ٱلَّذِينَ أُوتُوا۟ ٱلْكِتَٰبَ لَيَعْلَمُونَ
أَنَّهُ ٱلْحَقُّ مِن رَّبِّهِمْ ۗ وَمَا ٱللَّهُ بِغَٰفِلٍ عَمَّا يَعْمَلُونَ ﴿١٤٤﴾

> *Basi geuza uso wako upande wa msikiti Mtakatifu (Al-Ka'aba) na popote mnapokuwa zielekezeni nyuso zenu uliko (msikiti huo). Na hakika wale waliopewa kitabu (Mayahudi) wanajua kwamba hiyo ni haki itokayo kwa Mola wao; na Mwenyezi Mungu si mwenye kughafilika na yale wanayoyatenda. (2:144)*

Mabadiliko ya Qibla yaliashiria kuhamishwa uongozi toka kwa Wayahudi kwenda kwa Waislamu. Walijua kuwa Waislamu sasa wanapewa uongozi wa kuamrisha mema na kukataza maovu, kazi ambayo Wayahudi walikuwa wameshindwa kuitekeleza. Hivyo, Wayahudi walichukizwa sana wakashirikiana na wanafiki katika kujaribu kuwafanya Waislamu waone mabadiliko hayo ya Qibla si kitu kizuri kwa kusema:

**Inakuwaje wakati mmoja watu wanaelekea huku (Yerusalemu) na halafu wakati mwingine wanabadilisha tena na kuelekea huku (Ka'aba).**

Jambo jengine lililowachukiza sana wayahudi ni tamko la Qur-an kuwa kwa hakika ni Waislamu ndio watu ambao wanaifuata kikweli dini aliyoifuata pia Nabii Ibrahimu (a.s). Wayahudi walikuwa wanaamini kuwa watu wote wamepotea isipokuwa Wayahudi, na kwamba ni Wayahudi peke yao ndio wanaofuata dini aliyoifuata Nabii Ibrahimu (a.s). Na kwamba Nabii Ibrahimu mwenyewe alikuwa ni Myahudi. Madai hayo yanakanushwa na Qur-an. Kwa mfano katika Qur-an 3:67 – 68 Mwenyezi Mungu anasema:

مَا كَانَ إِبْرَٰهِيمُ يَهُودِيًّا وَلَا نَصْرَانِيًّا وَلَٰكِن كَانَ حَنِيفًا مُّسْلِمًا
وَمَا كَانَ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿٦٧﴾ إِنَّ أَوْلَى ٱلنَّاسِ بِإِبْرَٰهِيمَ لَلَّذِينَ
ٱتَّبَعُوهُ وَهَٰذَا ٱلنَّبِىُّ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ ۗ وَٱللَّهُ وَلِىُّ ٱلْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٨﴾

*Ibrahimu hakuwa Myahudi wala Mkristo, lakini alikuwa mwongofu, mtii, na wala hakuwa katika washirikina. Watu wanaomkaribia zaidi Ibrahimu ni wale waliomfuata yeye na Mtume huyu (Muhammad) na waliomwamini. Na Mwenyezi Mungu ndiye mlinzi wa wenye kuamini. (3:67-68)*

Hivyo kadiri Uislamu ulivyopata nguvu ndivyo Wayahudi walivyozidi kuchukia na wakawa wanautumia mkataba wa Madinah uliowapa haki na uhuru wa kukaa na Waislamu kwa amani kama silaha ya kuuhujumu Uislamu. Walianza kuzidhihirisha chuki zao kwa kumdhihaki Mtume na Waislamu, kuwanyanyasa na kuwafanyia ufedhuli Waislamu.

Hivyo dola changa ya Kiislamu ya Madinah ilikabiliwa tangu mwanzo na maadui wakubwa watatu walioshirikiana bega kwa bega katika kuuhujumu Uislamu. Maadui wa ndani walikuwa ni wanafiki na Wayahudi na maadui wa nje walikuwa ni Maquraishi wa Makkah.

## Upinzani dhidi ya dola ya kiislamu

### 1.Vita vya Badr

Maquraishi waliwafanyia Waislamu vitimbi mbali mbali ili kuudhoofisha na hatimaye kuufutilia mbali Uislamu. Lakini hawakufaulu. Walipanga njama za kumwua Mtume, nazo pia zilifeli na Mtume (s.a.w) alihamia Madinah. Makafiri wa Makkah walichukizwa sana na uhuru waliokuwa nao Waislamu walipohamia Madinah na walihofia kuwa Uislamu utapata nguvu. Wakafanya kila njia katika kuihujumu Dola hiyo changa. Hilo liliposhindikana walianza kuuhujumu uchumi wa serikali ya Kiislamu ya Madinah kwa kuiba mifugo, na kuchoma moto malisho ya wanyama na viunga vya mitende. Kuwaua walinzi wa mifugo na kuchoma nyumba moto. Muda wote huo Waislamu walikuwa hawajapewa na Mwenyezi Mungu idhini ya kupigana kijeshi na makafiri. Makafiri walipoendelea kuwabughudhi Waislamu hata baada ya kuhamia Madinah Mwenyezi Mungu akawapa idhini Waislamu kupigana:

أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقَٰتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظُلِمُوا۟ ۚ وَإِنَّ ٱللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ ﴿٣٩﴾ ٱلَّذِينَ أُخْرِجُوا۟ مِن دِيَٰرِهِم بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّآ أَن يَقُولُوا۟ رَبُّنَا ٱللَّهُ ۗ

*Wameruhusiwa (kupigana) wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa. Na kwa yakini Mwenyezi Mungu ni muweza wa kuwasaidia. Na ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki ila kwa sababu wamesema: Mola wetu ni Allah … (22:39-40)*

Idhini hiyo pia ilitolewa katika aya nyingine kama vile 8:39, 2:190, 2:190-193 na 9:13, 15. tukizingatia aya hizo tunajifunza kuwa Waislamu wanayo haki na wajibu wa kupigana kwa madhumuni yafuatayo:

**(1)Kujihami dhidi ya mashambulio ya maadui.**

Sababu ya kwanza ni kujilinda waislamu dhidi ya mashambulizi yanayofanywa na kikundi au taifa lolote. Yanapotokea mashambulizi, waislamu wanahaki ya kujitetea maisha yao, na hususani, kulinda maisha ya watoto, wanawake, wagojwa na wazee, pamoja na viumbe vyengine vya Allah(s.w).

**(2)Kuondoa fitina katika jamii.**

Makusudio ya fitina hapa ni ama kuwanyima Waislamu haki na uhuru wao wa kuufuata Uislamu; au kuwazuia watu wengine wasiwe Waislamu, au kuwazuia Waislamu haki yao ya uhuru wa kuutangaza Uislamu.

**(3)Kuondoa dhulma na uonevu.**

Uislamu ni dini ya amani. Na amani haiwezi kuwepo katika jamii iliyojaa dhulma na uonevu. Hivyo mahali penye dhulma na uonevu Waislamu wana haki na wajibu wa kupigana kuiondoa dhulma hiyo. Hivyo makafiri wa Makkah walipoendelea na hujuma zao, Waislamu waliamua kuingia vitani ili kujihami. Katika vita vya mwanzo vilivyopiganwa katika eneo la kijiji cha Badri, kilichopo maili 80 hivi nje ya mji wa Madinah, jeshi la Waislamu lilikuwa na askari 313, farasi 2 na ngamia 70 tu wakati jeshi la makafiri wa Makkah lilikuwa na ubora za zana bora za kivita. Katika vita hivyo vya Badri vilivyotokea mwezi wa Ramadhani katika mwaka wa 2 A.H. Waislamu kwa msaada wa Allah waliwashinda vibaya makafiri. Na ushindi mkubwa wa Waislamu katika vita hii ulileta athari kubwa tatu:

**Kwanza,** ushindi mkubwa wa Waislamu ulikuwa ni dalili na kielezo kuwa Uislamu ni dini ya Allah na ushindi wao ni matokeo ya msaada waliopewa na Allah.

**Pili,** ushindi huo uliwapa nguvu, hamasa na matumaini makubwa Waislamu ya kuusimamisha Uislamu na kuufanya uwe juu ya dini zingine zote.

**Tatu,** ushindi huo pia uliwafanya maadui wa Uislamu watambue kuwa Uislamu ni nguvu kubwa yenye uwezo wa kujitetea dhidi ya maadui zake na hivyo kuiogopa na kuiheshimu.

**2.Njama za Wayahudi dhidi ya Waislamu**

Kama tulivyokwishaona vita vya badri vilikuwa ni mbinu mojawapo ya upinzani dhidi ya dola ya Kiislamu iliyotumiwa na makafiri wa Makkah. Upinzani huo ulijitokeza pia katika sura nyingine. Njama za Wayahudi za kutaka kumuua Mtume (s.a.w) na kuudhoofisha Uislamu kwa vitimbi mbali mbali. Baadhi ya vitimbi hivyo ni hivi vifuatavyo:

(a) Kutangaza kuwa Muhammad (s.a.w) ni Nabii wa uongo.

(b) Kuifanyia Qur-an stihizai.

Kwa mfano Mwenyezi Mungu aliposema katika Qur-an 2:245: "Jee, ni nani ambaye atamkiridhi Mwenyezi Mungu kardha njema, iwe ni sababu ya yeye kumzidishia ziyada nyingi?" Mayahudi wakawa wakipita mitaani wakinadi kuwa Mwenyezi Mungu fakiri na wao matajiri!

(c) Kumjaribu Mtume (s.a.w) kwa maswali.

Kwa kumuuliza maswali magumu yasiyokuwa na majibu ya dhahiri. Baadhi ya maswali waliyouliza ni Mwenyezi Mungu kaumbwa na nani? Au roho ikoje na inakaa wapi? Kiyama kitakuwa lini? Usingizi wako ukoje? Ni vitu gani Israili alijiharamishia mwenyewe na kwa nini? n.k.

(d) Kuwavunja moyo na kuwadhihaki Waislamu.

(e) Kuwachochea na kuwatenganisha Waislamu.

(f) Kushirikiana na wanafiki katika njama za kutaka kumuua Mtume (s.a.w).

(g) Walidhihirisha usaliti wao baada ya ushindi wa Waislamu katika vita vya Badri.

Katika kukabiliana na njama za Wayahudi dhidi ya dola ya Kiislamu, Mtume (s.a.w) alichukua hatua kubwa mbili; kwanza aliwahukumu adhabu ya kifo watu waliokuwa wakiongoza uchochezi huo, na pia kuendesha vita vya Banu Qainuqa, Banu Nadhir na Banu Qaraizah.

**2. Vita vya Uhd**

Baada ya kushindwa vibaya katika vita vya Badri; makafiri walihuzunika sana na wakaanza kujiandaa kwa vita vingine ili walipize kisasi cha kuuliwa kwa makafiri wengi katika vita vya Badri. Hindu binti Utbah, mke wa Abuu sufiyani kwa mfano alikula kiapo kuwa endapo Hamza atauliwa basi atakula moyo na ini la Hamza. Na kweli alikuja kutimiza ahadi yake hiyo japo alishindwa kulimeza. Makafiri waliandaa jeshi la askari 3,000 askari 700 kati ya hao walivaa mavazi ya chuma. Jeshi hilo pia lilijiandaa kwa silaha nyingi zilizo bora.

Waislamu ambao walikuja kujua juu ya mpango huo wa vita siku tatu tu kabla ya kuanza waliandaa jeshi la watu 1000. Na kati ya hao askari 300 wanafiki wakiongozwa na Abdullah bin Ubay walijiengua kabla ya vita kuanza na kuamua kurejea Madinah kwa kisingizio cha Mtume (s.a.w) alilikataa na pendekezo lao la kutaka wapiganie ndani ya mji wa Madinah.Uwanja wa vita hivyo ulikuwa karibu na mlima wa Uhudi, na ndio maana vimepewa jina la vita vya Uhudi.

Baada ya vita hivyo kuanza Waislamu walielekea kupata ushindi mkubwa dhidi

ya makafiri. Lakini ushindi huo uligeuka pale walinzi wapiga mishale wapatao 50 wa jeshi la Waislamu walipoondoka katika sehemu yao ya ulinzi na kuanza kusherehekea ushindi na kugombea ngawira. Maadui walipoona walinzi wa jeshi la Waislamu wanaondoka katika ile sehemu muhimu ya ulinzi walitumia fursa hiyo kuwazingira na kuwashambulia Waislamu kwa nyuma.

Waislamu walijikuta wakipoteza ushindi wao na kuanza kusambaratika. Lakini Mtume (s.a.w) aliwaunganisha askari wachache waliokuwapo na kuanzisha mashambulizi upya hadi makafiri wakakimbia. Waislamu wakajikusanya upya na kuwafukuza maadui hao. Na hawakurejea hadi makafiri walipotokomea kabisa.



**Mafunzo yatokanayo na vita vya Uhudi**

Miongoni mwa mafundisho makubwa tunayoyapata kutokana na vita hivyo ni haya yafuatayo:

(1) Kabla ya kuanza vita, Mtume (s.a.w) alishauriana na Waislamu juu ya namna bora ya kupambana na adui na akaufuata ushauri wa uliofaa. Hapa tunajifunza umuhimu wa kushauriana katika mambo. Huo ndio Uislamu wa kweli.

(2) Ingawa Waislamu wameahidiwa ushindi na Allah, ahadi hiyo haina maana kuwa Waislamu waweza kupigana bila kupanga vizuri mbinu za midani ya vita. Ndio maana Mtume (s.a.w) alilipanga vizuri sana jeshi lake na hivyo kuwawezesha Waislamu kupata ushindi mapema.

(3) Kugeuka ghafla kwa ushindi wa Waislamu kunatufundisha siyo tu umuhimu wa kufuata vizuri mbinu za vita, bali tunajifunza umuhimu na ulazima wa kutii amri tunazopewa na viongozi.

(4) Kama ilivyokuwa katika vita vya Badri, katika vita vya Uhudi pia tunajifunza kuwa ushindi katika vita hautegemei uwingi au ubora wa silaha, bali ushindi siku zote ni wa wale wanaoshikamana na maamrisho ya Allah, na kumtegemea Yeye tu.

**Athari za Vita vya Uhudi**

Kutetereka kwa Waislamu katika vita vya Uhudi kuliwafurahisha sana Wayahudi na wanafiki na kukawatia nguvu ya kuzidisha upinzani wao dhidi ya Dola ya Kiislamu. Baada ya vita vya Uhudi upinzani wa maadui wa Uislamu ulichukua sura mbali mbali. Baadhi ya mbinu zilizotumiwa na maadui ni hizi zifuatazo:

**(i) Hila za Ulaghai**

Ilipowadhihirikia makafiri kuwa Waislamu ni wapiganaji madhubuti na si rahisi kuwashinda kwa kutumia nguvu za kijeshi, wakaanza kuwahujumu Waislamu kwa kutumia hila za ulaghai. Kwa mfano kiongozi wa kabila la Kilab aitwaye Abu Bara bin Malik-al-Kilab alimwendea Mtume (s.a.w) na kumwomba ampatie Waalimu watakaokwenda kufundisha Uislamu kwa watu wake. Mtume alilipokea ombi hilo kwa moyo mkunjufu na akawateua waalimu 70 walio wazuri kabisa na kuwatuma waende huko. Walipofika huko walikamatwa na kuuliwa.

Aidha, watu wa kabila la adal na Qaral walimwomba Mtume (s.a.w) awapatie walinganiaji watakaokwenda kuufundisha Uislamu kwa watu wao. Awaliwapatia wanazuoni 10 chini ya uongozi wa Asim bin Thabit. Nao pia walikamatwa na kuuliwa. Matukio haya yaliwahuzunisha sana Waislamu.

**(ii)Kuwafitinisha Waislamu**

Mbinu nyingine waliotumia maadui katika jitihada zao za kuuhujumu ilikuwa ni ya kujaribu kuwafitinisha Waislamu ili wasiwe kitu kimoja kwa kutumia ubaguzi wa kikabila na nasaba. Mbinu hii aliitumia sana kiongozi wa wanafiki Abdullah bin Ubay kwa kujaribu kuwachochea Waislamu waliozaliwa Madinah yaani Answaari wawachukie Waislamu wenzao waliohamia Madinah kutoka Makkah, yaani Muhajiriina.

**(iii)Uzushi dhidi ya bibi Aisha (r.a)**

Mbinu nyingine waliyoitumia ili kumwudhi Mtume (s.a.w) na kuwavunja moyo Waislamu ilikuwa ni kumzulia Mke wa Mtume (s.a.w) Bibi 'Aisha kuwa ametenda kitendo kiovu cha zinaa kwa lengo la kuupaka matope Uislamu ili watu wauchukie kwa kuuona kuwa hauna maana.

**Vita vya Ahzab**


Banu Nadhir waliondoka Madinah walieneza chuki na uadui dhidi ya Waislamu. Waliwachochea makafiri wa Makkah na kuwahimiza waandae shambulio kubwa kabisa la kivita litakaloufutilia mbali Uislamu. Na wao walijitolea mali zao nyingi ili kufanikisha jambo hilo. Waislamu walipopata habari juu ya mpango huo wa kuwashambulia waliamua kujihami kwa kuchimba handaki lenye upana wa mita tano na kina cha mita tano kuzunguka mji wa Madinah. Pendekezo la kuchimba handaki lilitolewa na Salman al-Farsy. Waislamu walizingirwa na maadui kwa muda wa mwezi mmoja hivi. Lakini waliweza kujihami na kupambana na maadui, kwani handaki walilolichimba liliwasaidia sana.

Hali ilikuwa ngumu sana kwa Waislamu hasa kutokana na uhaba mkubwa wa chakula uliokuwa ukiwakabili wakati wote. Lakini waliendelea kusubiri. Wayahudi Banu wa Quraizah walikuwa Madinah na ambao walikuwa na mkataba na Waislamu waliwasaliti Waislamu baada ya kushawishiwa na Banu Nadhir. Wakaungana na makafiri katika kuwapiga vita Waislamu. Hata hivyo Mtume (s.a.w) haraka alipeleka jeshi la kudhibiti usaliti wao huo.

Baada ya kuonyesha subira na ujasiri wa kupambana na makafiri, Mwenyezi Mungu aliwateremshia waislamu rehema zake kwa kuleta upepo mkali

ulioandamana na mvua kubwa ukayang'oa mahema ya makafiri, wakakimbia kwa hofu na mashaka.

Baada ya hapo, majeshi ya Waislamu yaliwakabili wayahudi wa Banu Quraizah ili kuwaadhibu. Wakapewa adhabu waliyoipendekeza wao wenyewe kwa mujibu wa mafundisho ya Taurati kama yalivyo katika Kumbukumbu la torati 20:10-15 kuwa wanaume wauliwe lakini wanawake na watoto wachukuliwe mateka.




## Mkataba wa Hudaibiya

Kama tulivyokwisha kuona katika maelezo yaliyotangulia, tangu kuhamia Madinah, Waislamu hawakupata fursa ya kukaa kwa amani na utulivu, kutokana na kubughudhiwa na makafiri. Mwaka wa 6 A.H. Mtume (s.a.w) aliota

amenyoa nywele baada ya Hija. Akaamua kwenda kufanya Umra mwezi wa Dhul-Qa'adah mwaka wa 6 A.H. akiwa ameongozana na Waislamu 1400 wasio na silaha. Makafiri wa Makkah waliwazuia kuingia Makkah na hivyo Waislamu wakapiga kambi katika kitongoji cha Hudaibiya, huku wakifanya jitihada za kufikia makubaliano nao. Baada ya majadiliano ya muda mrefu hatimaye mkataba wa amani wa miaka kumi uliojulikana kama mkataba wa Hudaibiya ulifikiwa baina ya Waislamu na makafiri. Makubaliano ya mkataba huo uliotiwa saini na Mtume (s.a.w) kwa niaba ya Waislamu na Suhail bin Amr kwa niaba ya makafiri yalikuwa kama ifuatavyo:

(i) Waislamu warudi Madinah bila ya kufanya Umrah mwaka ule.

(ii) Waislamu wanaweza kurudi mwaka uliofuata (7:A.H) kufanya Umra lakini wakae Makkah siku tatu.

(iii) Wakija Makkah wasije na silaha ila panga zikiwa ndani ya ala zao.

(iv) Waislamu wasiende nao Madinah Waislamu wanaoishi Makkah na wala hawatamzuia yeyote miongoni mwao anayetaka kubakia Makkah.

(v) Kama yeyote wa Makkah atatoroka kwenda madinah kusilimu Waislamu hawana budi kumrudisha (wasimpokee), lakini yeyote kutoka Madinah akitoroka kwenda Makkah kuritadi, Maquraishi hawatapaswa kumrudisha Madinah (watampokea).

(vi) Makabila ya Waarabu watakuwa huru kufanya urafiki na upande wowote ule wautakao.

(vii) Pasiwe na vita kwa kipindi cha miaka kumi baina ya Waislamu na Maquraishi na baina ya marafiki wa Waislamu na marafiki wa Maquraishi.

(viii) Hapana ruhusa ya kutengua hata sharti moja katika hizi kabla ya miaka 10 kupita.

Ingawa mkataba huo ulionekana kuwabana sana Waislamu, lakini ulikuwa ni wenye kuleta ushindi mkubwa kwa Waislamu.

**Kwanza** wale Waislamu waliotorokea Madinah ili wakapate hifadhi na utulivu wa kumcha Mungu wao hawakuridhika kabisa kurudi tena Makkah. Na kwa kuwa walirejeshwa kwa mabavu waliamua kutoroka na kuishi porini na

kuishambulia na kuipora misafara ya biashara ya makafiri wa Makkah. Baada ya muda mfupi watu hao wakawa kero kubwa sana hadi Maquraishi wenyewe walimwomba mtume (s.a.w) awapokee watu hao ili wawe chini ya udhibiti wa Mtume (s.a.w).

**Pili**, mawasiliano baina ya Waislamu na makafiri yalitoa fursa nzuri kwa makafiri kujionea wenyewe ubora wa Uislamu na hivyo kuwapeleka wengi wao kusilimu.

Kwa mfano, katika kipindi cha miaka miwili tu ya mkataba huo walisilimu watu wengi kuliko waliowahi kusilimu katika miaka yote ya nyuma.

**Tatu**, mkataba huo wa amani uliwapa fursa nzuri Waislamu ya kuwafikishia wasiokuwa Waislamu ujumbe na mafundisho ya Uislamu. Walitoa mafunzo hayo kwa waliokuwa jirani nao na hata waliokuwa katika nchi za mbali. Na ni katika kipindi hiki ambapo Mtume (s.a.w) aliwapelekea barua wafalme wa Urumi, Uajemi, Misri, Yemen, Shamu, Uhabeshi na Bahrain.

### 4. Vita vya Khaibar

Wayahudi waliokuwa wakiishi Khaibar, umbali wa maili 200 hivi kaskazini mwa Madinah walipanga njama za kuishambulia Madinah. Mtume (s.a.w) alilizima jaribio hilo kwa kuwapelekea jeshi la Waislamu 1600 katika mwezi wa Muharamu 7 A.H. na kuwashinda. Na Wayahudi hao wakaachwa huru kwa makubaliano na kulipa fidia ya nusu ya mazao yao ambayo wangevuna mwaka ule. Pamoja na kupewa msamaha huo, wayahudi hao wakapanga njama za kumwua Mtume (s.a.w) kwa kumtilia sumu kwenye chakula. Lakini Mwenyezi Mungu alimnusuru na njama hizo.

### Waislamu waenda Umrah

Mwaka uliofuata baada ya mkataba wa Hudaibiya, Waislamu wapatao 2000 walikwenda kufanya Umrah ile waliyozuiliwa kufanya katika mwaka uliotangulia. Na miongoni mwa matunda ya safari hiyo ni kusilimu kwa watu wengi wa makkah baada ya Umrah hiyo.

### Vita vya Muttah

Bwana Harith aliyepewa barua na Mtume (s.a.w) kumpelekea mfalme wa Basra aliuliwa katika eneo la kitongoji cha Muttah kwa amri ya gavana mmoja wa Heraklas wa Urumi. Kitendo hiki cha kuuliwa mjumbe huyo kilimsikitisha

sana Mtume (s.a.w) na alituma jeshi la askari 3000. Lakini jeshi hilo likajikuta likilazimika kupambana na askari laki moja. Waislamu waliwashangaza warumi walivyoweza kupambana na jeshi hilo pamoja na uchache wao. Mapambano yalikuwa makali na Waislamu wengi walikufa mashahidi. Hata hivyo, Waislamu wachache waliobaki walipigana kijasiri kiasi ambacho Warumi waliogopa kuendelea na mapigano na Waislamu wakarejea Madinah.

**Kukombolewa kwa Makkah**

Japokuwa awali makafiri wa Makkah waliufurahia sana mkataba wa Hudaibiya kwa kuwa walihisi unawapendelea wao, baada ya muda mfupi wakawa wa mwazo kuuvunja mkataba huo kwani walijionea wenyewe jinsi mkataba huo ulivyowapa nguvu Waislamu. Walilolitarajia halikuwa. Hivyo wakaanza vitimbi vya kuwashambulia Waislamu na mali zao kwa hila na kujificha. Hali hiyo ikawa inaleta bughudha upya kwa Waislamu. Ili kuiondoa kabisa fitina hii, Mtume (s.a.w) aliandaa jeshi la askari 10,000 lililokwenda kuukomboa mji wa Makkah, Waislamu waliingia Makkah mwezi 10 Ramadhani, 8 A.H. na kuukomboa mji huo mtukufu pasi na upinzani wowote wa maana. Mara baada ya kuingia Makkah Waislamu walikwenda kuisafisha Ka'aba kwa kuyaondolea mbali masanamu yote yaliyowekwa humo.

Japokuwa makafiri wa makkah walikuwa wamewafanyia Waislamu ukatili na uadui mkubwa sana, ulipotekwa mji wa Makkah Mtume (s.a.w) aliwasamehe maadui zake wote na raia wote waliachwa wakae kwa amani. Kukombolewa kwa mji wa Makkah kulifuatiwa na kusilimu kwa wingi kwa watu wa makabila mbali mbali isipokuwa makabila ya Hawazin na thaqif ambayo yalikuja kusalimu amri baada ya vita ya Hunain.

**Msafara wa Tabuk**

Baada ya kukombolewa kwa Makkah, Uislamu ulipata nguvu na kuwa na wafuasi wengi. Nguvu hizi za Uislamu ziliwatia hofu viongozi wa dola za kikafiri zilizopatikana na Waislamu. Warumi wakawa wanaandaa jeshi la kuishambulia Dola ya Kiislamu. Mtume (s.a.w) alipopata habari hizi na kuzidhibitisha kuwa ni za kweli aliandaa jeshi la askari 30,000 ili kwenda kukabiliana na maadui hao.

**Msafara** wa Tabuk ulikuwa mtihani mkubwa wa kusafiri na hivyo kuhitaji masurufu makubwa zaidi na kujitolea zaidi.

**Pili,** amri ya kwenda Tabuk ilikuja katika kipindi cha joto kali sana na hivyo kuifanya safari hiyo ndefu kuwa ngumu zaidi.

**Tatu,** amri ya kwenda Tabuk ilikuja katika kipindi cha njaa kali, lakini pia karibu na mavuno kwani wakati huo mazao yalikuwa yanakaribia kuvunwa. Ugumu wa msafara huo ulikuwa ni mtihani uliowapambanua Waislamu waliokuwa na imani thabiti na waliokuwa tayari kuisadikisha imani hiyo kwa vitendo wakati wowote, na pia uliwadhihirisha wanafiki wanaotafuta visingizio vya kuhalalisha unafiki wao na pia wale Waislamu ambao japo si wanafiki lakini wazembe na si makini katika utekelezaji wa mambo.

Jeshi la Waislamu lilipiga kambi katika eneo la Tabuk kati ya Madinah na Damascus. Warumi waligwaya na kurudi ndani ya mipaka yao walipoliona jeshi la Waislamu kuwa lipo tayari kwa mapambano.

Baada ya siku 21 Waislamu walirejea Madinah kwa sababu lengo lao halikuwa kuivamia Urumi bali kuihami dola ya Kiislamu. Ujasiri ulioonyeshwa na Waislamu ulizidi kuyaathiri makabila ambayo yalikuwa bado kusilimu yafanye hivyo.

Baada ya kurejea kutoka Tabuk, Mtume (s.a.w) na Waislamu wote kwa ujumla walichukua hatua ya kuwarudia wale Waislamu walioonyesha uzembe kwa kutokwenda Tabuk. Kutokana na ulegelegele wa kupenda starehe kwao ilitolewa adhabu ya kuwasusia kwa kukata mawasiliano nao ikiwa ni pamoja na kutowatolea salamu au kushirikiana nao katika jambo lolote.

Hali hiyo iliendelea kwa muda wa siku 50 hadi Mwenyezi Mungu alipoteremsha aya ya kuwasamehe. Msafara huo wa Tabuk ulikuwa ndio msafara wa mwisho wa kijeshi alioufanya Mtume (s.a.w)

**Hija ya Kuaga na Kutawafu Mtume (s.a.w)**

Mwaka mmoja baada ya msafara wa Tabuk eneo lote la Bara Arabu lilikuwa chini ya dola ya Kiislamu, kwani watu walikuwa wakiingia katika Uislamu makundi kwa makundi. Na hiyo ikawa ni ishara kuwa kazi yake ya Utume imekaribia kwisha. Baada ya kukombolewa Makkah hija ya mwanzo ya mwanzo 9 A.H. iliongozwa na Abu bakar.

Mtume alifanya hija yake ya mwanzo na ambayo ilikuwa pia ya kuaga mwaka wa 10 A.H. na alitoka Madinah na zaidi ya watu 100,000. Katika uwanja wa

Arafa Mtume (s.a.w) alitoa hotuba ya kihistoria, hotuba ambayo ilitilia mkazo mambo mengi muhimu. Miongoni mwake ni haya yafuatayo:

(1) Aliwausia watu kumcha Mwenye Mungu wakati wote.

(2) Aliwakumbusha umuhimu wa kuheshimu na kulinda haki za watu, uhai wao, mali zao na heshima zao. Hizo ni haki muhimu zisichezewe.

(3) Kila mtu ataulizwa na kuhisabiwa kwa makosa au amali zake.

(4) Waislamu wote ni ndugu, wasioneane.

(5) Watu wajiepushe sana na riba kwani ni haramu.

(6) Aliwausia wanaume wakae na wake zao kwa wema na ihsani.

(7) Aliwahimiza Waislamu kuwatii viongozi wao.

(8) Aliwakumbusha Waislamu umuhimu na wajibu wa kuitekeleza sheria ya Kiislamu ya Mirathi kwa uadilifu.

(9) Aliwakumbusha watu wajiepushe na uchafu wa zinaa.

(10) Aliwahimiza pia wachukue hadhari kubwa na makosa madogo madogo kwani hayo baadaye humpelekea mtu kufanya makosa makubwa.

(11) Alisisitiza kuwa Waislamu hawatapotea ikiwa watashikamana na kuyafuata mafundisho na mwongozo uliomo katika Qur-an na Sunnah za Mtume (s.a.w). Baada ya kumaliza hotuba hii, siku hiyo hiyo ikateremka aya isemayo:

ٱلْيَوْمَ يَئِسَ ٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ مِن دِينِكُمْ فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَٱخْشَوْنِ ۚ
ٱلْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِى وَرَضِيتُ
لَكُمُ ٱلْإِسْلَٰمَ دِينًا

*"… Leo waliokufuru wamekata tamaa katika dini yenu, basi msiwaogope bali niogopeni mimi. Leo nimekukamilishieni dini yenu na kukutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe Dini yenu….". [5:3]*

Wiki mbili tu baada ya Hija hii ya kuaga Mtume alishikwa na ugonjwa wa kichwa na homa. Ugonjwa ulipozidi alimteua Abu Bakar aswalishe.

Siku nne kabla ya kutawafu kwake alipata nafuu kidogo na akaenda Misikitini lakini alimwacha Abu bakar aendelee kuswalisha. Baada ya swala hiyo Mtume (s.a.w) aliwahutubia waumini kwa kusema:

> **"Allah amempa mja wake achague kati ya dunia na akhera. Akachagua akhera. Ninawausia, Enyi Waislamu (Muhajirina) muwe wema kwa Ansar. Hakika wametekeleza wajibu wao vizuri. Waislamu kwa ujumla wao idadi yao itaongezeka lakini Answar watapungua na kuwa kama chumvi katika chakula. Zimeangamia umma zilizotangulia ambazo ziliabudu makaburi ya Mitume wao na ya watu wema. Ninawakatazeni kufanya hivyo. Nina deni kubwa (la Ihsani) kwa Abu Bakar. Kama ingekuwa nimfanye yeyote kuwa rafiki yangu, angalikuwa Abu Bakr, lakini uhusiano (udugu) wa Uislamu unatosha. Ee, binti yangu Fatimah na Ee, shangazi yangu mpendwa, Swafiyah, fanyeni amali kwa ajili ya akhera kwani sitaweza kuwasaidia chochote dhidi ya hukumu ya Allah.**

Hiyo ilikuwa hotuba yake ya mwisho na ilipofika mwezi 12 rabi'al-Awwal mwaka 11 A.H. sawa na tarehe 8 Juni 632 A.H. Mtume (s.a.w) alifariki dunia na kuzikwa siku iliyofuatia akiwa na umri wa miaka 63 kamili.



## Zoezi la Tano

1. Taja mambo matano aliyofanya Mtume (s.a.w) ili kuanzisha dola ya kiislamu.

2. Msikiti wa Mtume (s.a.w) ulitumiwa kwa kazi gani?

3. Orodhesha maadui wa dola ya kiislamu na mambo waliyofanya dhidi ya Uislamu.

4. Taja manufaa waliyopata waislamu baada ya mkataba wa Hudaibiya

5. (a)Taja vita ambayo maadui wote wa Uislamu walishirikiana kuvamia Dola ya Madina kwa lengo la kuisambaratisha.

   (b) Waislamu walichukua hatua gani za kujihami?

   (c)Je, walifanikiwa? Kwanini?

6. Katika hija ya kuaga, Mtume (s.a.w) aliwahusia nini Waislamu?

7. Kutawafu Mtume (s.a.w) kunatufunza nini?